

**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

- | | |
|--------------------------------------|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani. |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdilllah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38. Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44. Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45. Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46. Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47. Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49. Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51. Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54. Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55. Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad

Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nne – Tarehe 19 Juni, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika, (Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuweka mezani hotuba ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi, kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, Kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wajumbe wa kamati ya wenyeviti, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusiana na mswada wa fedha kama ulivyowasilishwa na serikali. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 80

**Athari za Kimazingira Zinazosababishwa na
Kampuni za Ujenzi Mbali Mbali**

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa wana kijiji wa Vitongoji Makaani pamoja na vijiji vya jirani katika Jimbo la Wawi, tangu zamani, sasa na hata baadae walitegemea na wataendelea kutegemea ardhi ya Makaani kwa ajili ya kilimo, ardhi ambayo tayari kwa kiasi kikubwa mazingira yake yamesaharibiwa kwa kuchimbwa mashimo makubwa ya kifusi *Environmental Degradation* sambamba na kuchafuliwa kwa mazingira hayo jambo ambalo linaathiri sana afya za wakaazi wa maeneo hayo. Kwa kuwa wanaosababisha athari hizo kwa kiasi kikubwa ni kampuni za ujenzi wa barabara toka nje ya Zanzibar.

Je, ni lini serikali itazilazimisha kampuni za ujenzi kutoa mfuko wa uhifadhi wa mazingira wa Afya ya Jamii *Health Reform Fund* kwa shehia husika.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali la Mhe. Mjumbe swali lake nambari 80, naomba na mimi nieleze masikitiko yangu juu ya uharibifu wa mazingira, ambao umejitokeza katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, likiwemo eneo la Vitongoji na sehemu nyengine za Jimbo la Wawi, kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi kutokana na uchimbaji wa kifusi kwa ajili ya ujenzi wa barabara za nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo na masikitiko yangu, sasa kwa idhini yako naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, hivi karibuni imetayarisha Kanuni ya Usimamizi wa Maliasili zisizorejesheka, ambayo inatoa masharti ya mtu yeyote atakayepewa ruhusa ya kuchimba maliasili zisizorejesheka ikiwemo kifusi, kutayarisha mpango wa kuyaendeleza mashimo na kutekeleza mpango huo baada ya uchimbaji. Hivyo, serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, itajitahidi kusimamia kanuni hizo ili kuhakikisha kuwa hakutakuwa na mashimo mapya yatakayoachwa bila ya kuendelezwa hapa nchini.

Aidha, marekebisho ya Sheria ya Mazingira ambayo tunategemea yatazingatia kuweka kifungu cha yeyote atakayeharibu na kuchafua mazingira kuwajibika na uharibifu na uchafuzi huo wa mazingira (*polluter pay principle*).

Mhe. Spika, Sambamba na hilo, Kampuni ya Ujenzi ya *H-YOUNG Co. Ltd.* ambayo hivi sasa ipo kwenye eneo la Vitongoji inaendelea na shughuli za uchimbaji, kabla ya kuanza shughuli hiyo, kupitia ofisi yetu ya Idara ya Mazingira Pemba, tuna makubaliano ya kulifukia eneo baada ya uchimbaji.

Aidha, kampuni hiyo imeahidi kulifukia eneo ambalo limeachwa wazi na Kampuni ya *PRISMO* mwaka 2006 wakati wa kujengwa barabara ya Mkoani. Ni matumaini yetu kuwa baada ya ufukiaji huo wananchi wataweza kuendelea na shughuli zao za kilimo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa kuwa katika swali langu la msingi nilieleza kwamba ardhi ile ilikuwa ni tegemeo la maisha kwa watu wa Vitongoji na maeneo mengine yaliyopakana nayo kama vile Uwandani, Kibokoni, Wawi, Mjengo wa Banda na kadhalika. Kwa kuwa ardhi ile sasa hivi tayari imepoteza mbolea yake yote, haifai tena kwa shughuli za kilimo, hata kama hao *H. YOUNG. Co. Ltd* watafukia hayo mashimo, suala hilo itakuwa sio rahisi kuendeleza kwa kilimo.

a) Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wale waliotegemea kilimo cha Makaani katika shughuli za kimaisha, ili na wao waendeleo kujipatia riziki kwa upande mwengine, ukiachilia mbali kilimo ambapo ardhi yake mmeshaichafua.

b) Katika swali langu la msingi nilieleza kwamba mbali ya ile *Environmental Degradation*, yaani uharibifu wa mazingira. Vile vile Baraza la Mji wa Chake Chake wanatupa taka chafu sana, zikiwemo za hospitali, wanatupia pale pale Makaani na kuzichoma moto, wanapochoma moto inakuwa moshi mzito sana kiasi ambacho watu wengi wanaathirika kwa pumu na vifua katika eneo hilo la Vitongoji.

Je, wewe ofisi yako ikishirikiana na bwana mwenye dhamana ya mambo ya Mabaraza ya Mji, mna mpango gani wa kuwasaidia huduma ya afya wakaazi wa Vitongoji wale walioathirika na mambo ya pumu, vifua na vikohozi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Mjumbe ameeleza kwamba ana wasiwasi kuwa hata na maeneo ya Vitongoji yakirudishiwa kujazwa yale mashimo, wasi wasi wake ni kwamba hakutakuwa na mbolea ya kuweza wananchi wa eneo hilo ambao walikuwa wanalitegemea sana kuweza kuendeleza kilimo.

Hili ni suala ambalo linahitaji utafiti, kwa sababu Mhe. Spika, sisi tuna *evidence* ambayo inaonesha kwamba katika eneo la Uwandani Pemba, ambapo baadhi ya mashimo yaliyoachwa wazi baada ya kukata miamba iliyotoa matofali yamefukiwa, na kwa bahati nzuri sana eneo hilo sasa limekuwa ni eneo zuri sana kwa kilimo, sehemu ambayo migomba ilikuwa haistawi na mipapai, sasa inastawi pamoja na miti mingine ambayo ni ya mazao. Kwa hivyo, ni suala ambalo kwa kweli hatuwezi kujua katika eneo hili la Vitongoji kama hali itakuwa hiyo. Lakini nasema ni suala ambalo kwanza tuweze kurudishia angalau uhalisia wa eneo lile, baadae kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili tutaweza kufanya utafiti kujua labda kuna matumizi gani.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kanuni zetu zinatutaka tunaposema humu tuwe na uhakika wa kile tunachokisema. Katika hili ni kwamba wanaokata matofali kule Uwandani wao wanakata matofali wanachukua yale mawe, lakini hawa wanaochukua kifusi kwa kuchimba, wanachukua ile *top layer* ya udongo ambao ume-*contain organic matter*. *Scientifically* ile ndio *fertile soil* ile ya juu na ile ya chini inakuwa haina mbolea, kwa hivyo sio

rahisi. Kwa hivyo, huwezi kulinganisha wanaokata matofali kule kwa sababu wao wanachukua ule mwamba tu ile *top layer* wanaiacha pale pale, ambayo ndio iliyo-*contain organic matter scientifically* wakiacha pale kilimo kinakua. Lakini kwa ardhi ya Makaani, kwa sababu kifusi kinachukua *top layer*, haiwezi kuwa nzuri kwa kilimo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nipokee taarifa ya kitaalamu sana ya Mhe. Saleh Nassor Juma. Lakini nimuombe pia asiwe na papara asikilize jibu kwanza. Mimi nimempa mfano wa Uwandani na nilimwambia na naendelea kusema kwamba suala hili ni la kitaalamu na lithitaji wataalamu kwenda kuona baada ya mashimo hayo kujazwa, kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili yataweza kutumika tena kwa shughuli za kilimo. Sikusema moja kwa moja kwamba yakijazwa mawe yatakuwa ni yenye rutuba.

Mhe. Spika, nafahamu tofauti iliopo kati ya ukataja matofali *top layer* inarejeshwa pale na kati ya uchukuaji wa kifusi ambayo hiyo *top layer* yenyewe imeondoshwa. Kwa hivyo, nilimwambia kwamba kama anavyoeleza mwenyewe, suala hili ni la kitaalamu na lithitaji zaidi wataalamu wa kilimo, ili kulishughulikia. Naomba sana awe mvumilivu kusikiliza yale majibu.

Mhe. Spika, kuhusu suala lake la pili, kwa kweli suala hili la Baraza la Mji kuyatumia maeneo haya kwa utupaji wa taka. Nia yake inawezekana ilikuwa ni kuweza kutumia kama kuyajaza haya mashimo ambayo yako wazi. Lakini kama kumejitokeza hali hii ya uchomaji wa taka na athari kuweza kuifikia jamii. Nimuombe kwamba ofisi yangu kwa kushirikiana na Mabaraza ya Miji, tutaweza kwenda kuliona na kuweza kuona vipi wananchi wetu hawatoathirika na hali hiyo, ambapo tayari kuna wagonjwa wa pumu na hali kama hiyo na maradhi mengine inaweza kuyasababishia maradhi haya yakawa mabaya zaidi.

Pili namuahidi kwamba tutalishughulikia kuona kwamba athari haitokei kwa wananchi, na kama kuna hali hiyo basi iweze kusimamishwa mara moja kwa manufaa ya afya za wananchi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini kwa kuwa wizara yake ndio muhusika mkuu na usimamizi wa mazingira, na kwa kuwa katika maeneo yetu ya kando kando za mashariki sisi tuliokuwa katika sehemu za mawe ndio waathirika wakubwa wa uharibifu mkubwa huu wa mazingira. Kwa kuwa makampuni yanapokuja kuchimba kifusi kwa ajili ya kutengeneza barabara huwa kuna masharti wanapewa, ya kuwa baada ya kumaliza kuchimba wafukie. Lakini

makampuni hayo yanapotaka kujenga huwa yanakuwa rahisi kukubali, lakini wakati wanapochafua yale mazingira kurudisha inakuwa ni vigumu sana.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri, kwa kuwa yeye ndio msimamizi mkuu, atasimamiaje makampuni yaliopo sasa hivi yanayojenga barabara, hasa yanayochimba kifusi kule eneo la Micheweni, kwa sababu imeathirika vibaya sana. Je, atasimamiaje makampuni yale ya H. YOUNG.Co. Ltd. pamoja na MECCO, kuhakikisha kama mashimo yale makubwa yaliyochimbwa wanayafukia, ili angalau kupunguza ile hali ya mandhari ilioko.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika. Ni kweli kwamba maeneo haya hayapo Vitongoji tu na nilieleza kwenye jibu langu mama, kwamba maeneo mengi katika kuendeleza. Nataka tufahamiane kwamba wakati mwengine unayataka maendeleo, lakini usipokuwa makini unaingia katika uharibifu wa mazingira.

Mhe. Spika, ofisi yetu kwa kuliona hilo kwamba kulikuwa hakuna usimamizi mzuri wa kuingia mkataba na yule ambaye atachukua kifusi katika eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa barabara au shughuli nyengine za maendeleo. Nilieleza kwamba tumetengeneza sasa kanuni ambazo zitawabana sasa hawa ambao wanafanya shughuli hizi, ili kuhakikisha kwamba wanakwenda kulirejesha eneo lile angalau kuyajaza yale mashimo ambayo wamechukua kifusi.

Hivi sasa kabla ya kuanza shughuli yoyote basi tunaingia kwanza katika makubaliano na hawa ambao amewataja H. YOUNG. Co. Ltd. ambao wako kule kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Nimeeleza katika maelezo yangu kwamba tumekubaliana na watayajaza maeneo yale ambayo wao wamechukua kifusi.

Vile vile kwa kushirikiana na Wizara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka, lakini vile vile na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, tumeandaa mpango kwa pamoja kila mmoja kuainisha ni jinsi gani tutaweza kuyajaza mashimo haya ambayo yaliachwa awali sana, kwa sababu hakukuwa na kipengele madhubuti cha kuwabana hawa ambao walikuwa wanafanya shughuli za majenzi ya barabara.

Nam. 28

Uondoaji wa Dampu la Taka katika eneo la Darajani

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)

Nam. 15

Waheshimiwa Kulazimishwa Kutumia Sehemu ya VIP katika Uwanja wa Ndege

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni watumishi wa watu na wao ni sehemu ya jamii hiyo hiyo ya watu wanaowatumikia, na kwa kuwa kama Waheshimiwa nao ni wananchi na wao wanastahiki kupata huduma zote kwa usawa kama wanavyopatiwa wananchi wao wanaowatumikia.

a) Je, kwa nini Waheshimiwa Wawakilishi wanapopita Uwanja wa Ndege na kuonesha kitambulisho, wanalazimishwa kupita sehemu ya watu mashuhuri (VIP) ambako kuna malipo ya fedha ya Tshs. 20,000/=.

b) Je, kwa nini malipo ya (VIP) yamewekwa Tshs. 20,000/= ambazo sio kila mtu mashuhuri anaweza kuzilipa kwa ghafla moja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 15 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Baraza lako hili tukufu katika kipindi kilichopita limepitisha sheria ya kuanzisha kwa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege Zanzibar. Kabla ya hapo ilikuwa ni Idara ya Anga. Kwa hivyo, katika kuirekebisha ile Mamlaka, kuna mambo mengi imebidi yabadilishwe ikilinganishwa na Mamlaka za Wiwanja vya Ndege vilioko katika Afrika ya Mashariki na duniani kwa jumla.

Kwa hivyo, moja katika mabadiliko ambayo yametokezea ni kuifanya ile VIP, ambayo ilikuwa vile vile ni sehemu moja ambayo inatetewa sana kupita watu ambao wanastahiki tu, ili kuondoa dalili za kutumika vibaya. Lakini katika kuendesha mamlaka lazima kuna gharama.

Kwa hivyo, VIP kama viwanja vya ndege vyengine vilivyopo duniani imebidi ilipiwe. Kwa hivyo, nina ushahidi kamili kwamba Dar es Salaam wanalipisha VIP, Afrika ya Kusini wanalipisha VIP na kwengineko. Sasa hii ni kuifanya ile VIP iweze kutoa huduma zinazostahiki, na kwa sababu wanaopita pale ni Waheshimiwa, waheshimiwa tayari wana hifadhi yao, wana miko yao na wana heshima zao. Lakini ili kuifanya VIP kutokana na mfuko mdogo wa kuendesha mamlaka iweze kwenda, ni lazima Waheshimiwa waweze

kuchangia na kulipa ile siku ambayo yeye anataka kusafiri. Yule ambaye hasafiri halazimishwi kulipa, yule ambaye anatomia ile huduma ndio anayepaswa kulipa.

Ama kiwango cha Tshs. 20,000

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Mhe. Saleh Nassor Juma alizungumza hapa kwamba Mjumbe akitaka kuzungumza jambo ni lazima awe na uhakika nalo. Mimi mwenyewe yamenikuta nikalipishwa Shs. 20,000/- hivi juzi tu na risiti nitamletea. Kwa hivyo, anachozungumza Mhe. Waziri namuomba radhi sana, mimi namwambia azungumze kitu ambacho ana uhakika nacho na sikugusa chochote pamoja na kulipa Shs. 20,000/-.

Mhe. Spika: Hebu tuendeleo kusikiliza jibu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Sijamsikia Mhe. Spika, mimi.

Mhe. Spika: Jibu swali Mhe. Waziri, hili acha.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Shs. 20,000/- ni kiwango kidogo kilichowekwa kwa sababu hapo Dar es Salaam tu malipo ni dola 40. Kwa hivyo, hapa ni kiwango kidogo sana kilichowekwa kutokana na hali zetu zilivyo. Lakini pia Waheshimiwa ndio wanapita pale, sio lazima kila mtu ambaye anataka kupita aende pale ndio akalipe, watu wengine ambao hawatunii huduma ile, wanapita katika mlango wa kawaida hao hawalipi, wanapita ni huduma yao muhimu inayowekwa.

Mhe. Spika, na pale katika VIP kuna huduma ya kwenda mapema ukapumzika, ukapata pengine chai, mzigo wako unapelekwa, tiketi yako inakwenda kushughulikiwa. Sasa wale wafanyakazi wote waliokufanyia vile wanataka malipo, sasa malipo hayo yatatokea wapi na bajeti tunazipitisha sisi hapa wenyewe. Kwa hivyo, hicho ni kitu ambacho tunakiona duniani kote ndiko kulivyo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, wamezungumza Wajumbe wengi kwa kuona adhabu wanayoipata pale, ni ushahidi tosha ambapo mimi nimeshuhudia Wajumbe shida wanayoipata pale.

Mhe. Waziri huu uheshimiwa kesho upo na keshokutwa haupo, hiki ni kitu cha kupita tu na sisi wenyewe tunataka kufuata kama wapiga kura wetu kwa

kupitia pale. Mimi mmoja huwa situmii sana VIP, mpaka itokee dharura kuwe kuna Wataliana wengi pale ndio nitapita kule. Lakini Mhe. Spika, mimi pia yameshanikuta na kulazimishwa kupita VIP. Sasa Mhe. Waziri unaliambiaje Baraza hili.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mjumbe, hebu uliza swali kidogo kidogo kwa hisani yako.

Mhe. Spika: Rudia swali Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ushahidi tosha umeona mwenyewe Wajumbe walivyouliza hapa kuhusu suala hili linavyowakera Waheshimiwa Wajumbe wengine hata wakirudi safari Shs. 20,000/- za kulipa pale hawana. Sisi wengine tunataka kuchukua mfano kama wapiga kura wetu wanaotumia uwanja ule kwa kupitia kule kwa wanyonge, tusilazimishwe kupita VIP.

Je, Mhe. Waziri analiambia nini Baraza hili, kuwa sio lazima kupita kule au hiyo Shs. 20,000/- kupita kule VIP kama hukutumia maji ni lazima ulipe Shs. 20,000/- kukaa kwenye makochi tu yale, kuna umuhimu gani.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kama nimemfahamu, ni kwamba mtu anapokwenda VIP, anakwenda kwa yeye mwenyewe binafsi kwa sababu milango ni mbali mbali. Milango ya kupitia abiria wa kawaida ni mbali na milango ya VIP ni mbali. Yule wa VIP anatakiwa awe na kitambulisho kinachomuwezesha yeye kutumia ile VIP. Hata kama wewe ni VIP, yaani Mwakilishi au Waziri ukitumia kitambulisho cha Mzanzibari basi unaweza ukapita kule katika hali ya kawaida, wala hakuna atakayekuzuia. Kwa sababu wewe mwenyewe umeikataa ile huduma ambayo uliwekewa, kwa hivyo, sioni kama hapo pana mgongano wowote. Mtu ambaye hapendi kutumia huduma ya VIP, basi anatumia kitambulisho cha Mzanzibari anapita kule katika hali ya kawaida, wala halazimishwi kwamba wewe utatumia huduma ya VIP.

Lakini mara ukiingia kwenye huduma ya VIP, inabidi unasaini kitabu kile kinacholetwa na kwa hivyo unalazimika kulipa malipo ambayo yamewekwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi nakubaliana na utaratibu ulioanzishwa wa kulipa kodi katika eneo letu la Uwanja wa Ndege katika sehemu ya VIP, naunga mkono kwa taasisi ile kuanzisha utaratibu ule mzuri.

Lakini nataka Mhe. Waziri anisaidie swali dogo tu, kwa sababu inaonekana kunakuwa na mvutano na mmeshuhudia baadhi ya Waheshimiwa kuanza kuleta manung'uniko katika suala hili, huo utaratibu wenyewe ukoje? Kwa sababu baadhi ya Waheshimiwa wanaondoka kwa ndege ya saa 3:00 na kurudi ndege ya saa 6:00. Akiondoka kwa ndege ya saa 3:00 analipa Shs. 20,000/- na akirudi ndege ya saa 6:00 anatakiwa alipe Shs. 20,000/- Je, huu utaratibu ukoje?

Mhe. Spika, mimi nahisi atueleze huu utaratibu ukoje, yale malipo ni kila ukipita au kwa siku. Hii ndio hofu yangu au dhana yangu na ndivyo ilivyo. Kwa safari ya siku moja inakuwa ikoje Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nashukuru kwa Mhe. Mwakilishi kuuliza swali hili. Ni kweli wengi wana manung'uniko kwamba safari ingewekwa moja au ingewekwa ya kwenda tu. Lakini swali hili ukilizungumzia ni kwamba hatuna hakika sisi yule anayekwenda atarudia pale pale, kwa sababu kuna na maboti kwenye maeneo mengine. Pia alipokuwa anarudi hatuna hakika kwamba kumbukumbu zetu zimemuweka yeye kwamba ametumia kiwanja kile au hakutumia, hiyo ndio *argument* iliopo, kwa sababu hakuna uhakika wa kuwa atatumia kiwanja kile kwa wakati wa kurudi anatozwa kabisa, na kwa sababu kumbukumbu zetu haziweki, kwamba keshatumia uwanja huu leo asubuhi na mchana atatoa, hatuna kumbukumbu hizo mpaka sasa hivi. Kwa hivyo, madhali katumia atatoa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipatia nafasi asubuhi hii kuweza kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Mhe. Waziri kwanza unakubaliana na mimi kuwa nyinyi bado hamjajipanga?

Pili, Mhe. Waziri Shs. 20,000/- unaweza ukaniambia ni huduma gani ambazo inalingana na Shs. 20,000/- anapewa Mheshimiwa pale anapokuwa analipa.

Tatu, Mhe. Waziri huoni kama hii ni moja katika wizara yako kutia aibu kwa kiwango hiki ambacho unamtoza Mheshimiwa Mwakilishi au Mheshimiwa yeyote kuwa ni kiwango kikubwa sana, hata hakilingani na uwanja wa kimataifa mwengine.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza namshukuru kwa kuuliza swali, kwa sababu ni Mwenyekiti wangu wa kamati mpenzi sana. Lakini Mhe. Spika, bei inategemea na kitu kimoja wataalamu wanakiita *prestige*.

Mhe. Spika, kuna hoteli nyengine hiyo bei yake huwezi kuamini, kwa sababu unaweza kukaa hoteli nyengine siku 10 bei yake ni kwa siku moja au chakula chake ni kizuri zaidi kile cha kwenye hoteli nyengine kuliko kile utakachokinunua. Sasa ile *prestige* au ile hadhi kwamba wewe umetumia ule ukumbi ndio malipo yenyewe hayo. Kwa hivyo, ile bei usiilinganisha na kile ulichopewa tu, lakini ile hadhi kuwa umepokewa na umewekwa katika kochi Mhe. Spika, inatosha ile hadhi. Lakini swali lake la ‘b’ ni kwamba anasema sisi hatujajipanga.

Mhe. Spika, ni ushahidi ambao haufichiki kwamba Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kuna mabadiliko makubwa Mhe. Spika. Kwa mfano, pale nje tu gari zilikuwa hazina *parking*, na hivi sasa kuna *parking* ambayo ni madhubuti tena ina lami ndani na wala haina vumbi na taa zimo na wakati wowote mgeni anapofika anajua anakwenda wapi na mambo mengine ambayo Waheshimiwa Wajumbe wanaposafiri wanayaona. (*Makofi*)

Kwa hivyo, mambo mengine zaidi tutakuja kuzungumza kwenye kikao cha bajeti *Inshaallah* nakushukuru Mhe. Spika. (*Makofi*)

Nam. 2

Taaluma Kuhusiana na Magonjwa ya Miguu, Magoti na kadhhalika

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Kuna maradhi mengi yaliyoibuka kwa wingi hapa Zanzibar na miongoni mwa hayo ni maumivu na uvimbe wa miguu, maumivu ya magoti bila ya hata kuumia na maumivu ya nyonga mara kwa mara.

- (a) Je, Wizara ya Afya inatambua kuwepo kwa wingi wa wagonjwa hao na nini hasa chanzo chake.
- (b) Kama inatambua ni hatua zipi imechukua za kutoa taaluma ya kinga juu ya maradhi hayo na aina ya matibabu ya mwanzo kwa wale wenye dalili za kuugua.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tusikilizane Mhe. Haroun Ali Suleiman, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hija Hassan Hija tunaomba tuwe wasikivu kwa Mhe. Naibu Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

- (a) Wizara inafahamu na inatambua kuwepo kwa maradhi hayo. Sababu za maradhi hayo ni mtindo wa maisha ya kisasa, ambao umewafanya watu kuwa wavivu, hawatembezi kwa miguu, hawachangamshi miili yao na wala hawafanyi mazoezi ya viungo.
- (b) Mpangilio mbaya wa ulaji wa vyakula na hasa kupendelea kula vyakula vyenye mafuta, uwanga na sukari kwa wingi, ambapo husababisha unene (*obesity*)

Uzito wa mwili ambao hauendani na uwezo wa miguu na mgongo kuubeba.

Mabadiliko ya mifupa, viungo na moyo kutokana na watu kuishi kwa muda mrefu.

Hatua zilizochulikuwa na wizara ni kutoa taaluma ya kinga juu ya maradhi. Hatua zeneye ni hizi:-

- (i) Elimu ya Afya kwa jamii kupitia vyombo vyetu vya habari vya hapa nchini, redio, *TV* na magazeti.
- (ii) Kuhimiza watu kufanya mazoezi kila siku.
- (iii) Kuwaelimisha kuwa na mpangilio mzuri wa ulaji wao, kupunguza vyakula vya uanga, mafuta hasa ya wanyama, kutumia mboga za majani na matunda katika mlo wa kila siku.
- (iv) Elimu ya afya kwa mgonjwa, kumfahamisha aina ya maisha yanayotakiwa kuishi na miko anayotakiwa kujiwekea, ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo alilionalo kutokana na sababu nilizozitaja hapo juu.
- (v) Lakini ikishindikana kutibiwa kwa dawa zinazoweza kuondoa tatizo na kama kuna haja ya *operation* itafanyika kama tatizo limekuwa kubwa.

Mhe. Spika, napenda nichukue fursa hii niwapongeze baadhi ya watu ambao wamechukua juhudi kama Dkt. Mwana Omar na wenziwe wa ZADESA kwa hatua waliyoichukua kupitia Baraza la Michezo kwa kuanzisha Vikundi vya

Mazoezi ya Mwili kwa watu wa rika zote na jinsia zote. Kwa wale waliohamasika kufanya mazoezi wanayo nafasi nzuri ya kuepuka maradhi mengi ya sasa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika, kuna maeneo mengi ambayo yalioko mbali na huduma ya afya na maradhi haya hivi sasa yameshamiri. Je, ni lini serikali itaanzisha utaratibu wa kutoa huduma hii kwa maeneo yale ambayo wagonjwa hawawezi kuyafika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, matatizo haya sio kama yapo maeneo mengi tu, isipokuwa yapo nchi nzima, kwa sababu watu wote hivi sasa wameacha utaratibu wetu wa kizamani tuliokuwa tunaishi tukitembea hatupandi magari, na hivi sasa kila mtu anatembea kwa gari na wala sio kama kuna sehemu maalum.

Kwa mfano, ukiumwa na mgongo, ukizidi uzito na ukienda hospitali basi daktari yoyote yule wa kawaida anaweza kukusaili, kwa sababu hili sio jambo kubwa ambalo litashindwa kumuasa mgonjwa na dawa utapewa. Lakini pindipo pale suala limezidi uzito kwa yule daktari, basi yeye atakupeleka atakupa rufaa ya kwenda katika sehemu ambayo itahusika sasa kutatua tatizo lako, kwa sababu limeshafikia mbali. Lakini kama unakwenda mapema, basi daktari wa kawaida anaweza kukutibu.

Mhe. Mjumbe, anauliza kwa sababu najua tatizo analo na nilimpeleka na kumpa rufaa akaenda na akasaidiwa, kwa hiyo na wengi wote watakwenda kwa utaratibu huo huo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amezungumzia umuhimu wa suala la kufanya mazoezi, ili kuepukana na haya baadhi ya maradhi ambayo ameyataja.

Je, wizara yake anaonaje akashauriana na serikali kuu kubadilisha muda wa kufanya kazi ukaanza labda saa 2:00, ili watu asubuhi wakapata muda mzuri wa kufanya mazoezi.

Kwa maana hiyo, Wizara ya Afya ichukue bidii ya kushauriana na serikali kuweza kubadilisha muda wa kufanya kazi badala ya saa 1:30, ili kazi zianze

saa 2:00 na asubuhi watu waweze kupata muda mzuri wa kwenda kufanya mazoezi.

Mhe. Spika: Sina hakika kama ni swali la Wizara ya Afya, lakini majibu kama unayo Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kuhusu suala la muda sikusema kama lazima iwe asubuhi au usiku ama jioni. Kwa kweli mazoezi yanafanywa siku zote na ikiwa kama utafanya usiku itakuwa bora. (*Vicheko/Makofi*)

Mhe. Farida Amour Mohamed: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa baadhi ya watu wanasema kama maradhi haya yanasababishwa na mafuta ya kupikia ambayo hayana viwango. Vile vile kwa kuwa Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi inasimamiwa na Wizara ya Afya. Je, Wizara ya Afya ina mpango gani kwa watu wanaoleta mafuta haya ambayo hayana kiwango, ili kuzuia wananchi wa Zanzibar wasivamiwe na maradhi haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sina uhakika kama swali nimelifahamu. Lakini kama ni suala la mafuta naweza kulijibu, sasa sijui kama nitakuwa ninakujibu sahihi au laa.

Kwa kweli mafuta ya kupikia yako ya aina nyingi na yana sifa tofauti; kuna yale ambayo yenye *cholesterol* mengine haya, kuna ya miti au ya wanyama, yaani ni uchaguzi wa mtu binafsi. Lakini mafuta ambayo ni mazuri ni yale ya miti ambayo hayana *cholesterol*. Kwa hiyo, kuepuka hayo basi watu ingekuwa ni vizuri zaidi ikawa wanayatumia hayo mafuta ya miti.

Kwa mfano, *Sunflower* ni mafuta mazuri kwa kupikia na yamo tele, lakini haya mengine hayakatazwi kutumika, kwa sababu ukikosa *cholesterol*. Sasa kama kuna mtu anataka kuepuka hilo basi ninamshauri atumie mafuta ya *Sunflower* au mengine yoyote ambayo yameandikwa *cholesterol free*, kwa sababu kwenye kopo lile huwa kila kitu kimeandikwa. Mhe. Spika, kama mtu atakwenda dukani na hajui kusoma basi aseme anataka mafuta ambayo hayana *cholesterol* au lehemu kwa lugha ya Kiswahili na hayo akila atakuwa salama.

Nam. 147

Kesi za Ubakaji Kucheleweshwa na Vyombo vya Sheria

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Takwimu za kesi za unyanyasaji ikiwemo vitendo vya ubakaji za mwaka 2012 zinaonesha kesi 127 zilifunguliwa na kesi 66 zilisikikizwa na kutolewa hukumu ambapo watu watatu tu walipatikana na hatia.

- (a) Je, kwa nini kesi nyingi zinatupwa baada ya kufikishwa mahakamani.
- (b) Serikali imechukua hatua gani za kuhakikisha kesi hizo zinasimamiwa vizuri baada ya kufikishwa mahakamani, ili kuhakikisha haki ya kisheria inatendeka kwa waathirika wa matukio hayo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 147 kama ifuatavyo:-

- (a) Kesi zinafutwa zikifika mahakamani kwa sababu ya kukosa mashahidi au wahusika wenyewe huomba kesi zifutwe baada ya mapatano yao ya nje ya mahakama.
- (b) Mahakimu wamekuwa wakikumbushwa mara kwa mara kuwa maadili na kusimamia ipasavyo kesi za aina hiyo. Mahakimu hao pamoja na wahusika wengine kama vile Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Polisi, Wapelelezi, Wizara ya Afya na kadhalika, huwa wanakumbushwa kwa kuwa na vikao vya pamoja kwa kutafuta utaratibu mzuri wa kuzishughulikia kesi za aina hii.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri.

- (a) Hivi serikali imefanya utafiti gani kujua sababu gani za msingi kesi za ubakaji kwenda mahakamani na baadaye kufutwa na raia kuwa huru.

- (b) Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi inao wachunguzi wangapi bingwa wa kimataifa hasa katika makosa ya jinai yakiwemo ya unyanyasaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, sijui kama nimesikia vizuri. Siku zote tunasema kwamba kama hakuna ushahidi basi kesi haiwezi kwenda mahakamani wala mtuhumiwa hawezi kutiwa hatiani.

Tatizo kubwa ambalo tunalo na linaendelea ni kwamba kesi inaweza ikafikishwa mahakamani, lakini wazazi wa mhusika ndiye anayeomba kwamba kesi iondoshwe, kwa sababu wao wenyewe wameshakubaliana. Sasa kama hawa wahusika wakuu wameshasema hivyo huwezi tena kuipeleka kesi mahakamani, kwa sababu hata ukiwaita mashahidi kwa sababu wao ndio mashahidi wakuu na unapowaita hawaji, kwa hiyo ile kesi itatajwa tu shahidi haji.

Vile vile kuna sheria ambayo inayosema kwamba ikifika muda wa miezi minne kwa mfano kama shahidi hajapatikana au kesi haijaenda basi ifutwe. Kwa hivyo, sisi tunakwenda kwa mujibu wa sheria zinavyosema na hiyo ndio sababu moja kubwa.

Pili Mhe. Spika, baada ya kuona matatizo haya kama nilivyosema tumejaribu sana kuviita vyombo vyote vinavyohusika, ili kuwashawishi kwamba na wao wajaribu kuishawishi jamii, kwamba tunachotaka hapa si kusameheana hapa, lakini tunachotaka ni kumtia hatiani yule mtu ambaye amekosa.

Lakini mara nyingi huwa ninajaribu kusema sijui jamii itawatizama vibaya na nini, sasa hayo ni mambo ya kijamii na wala hatuwezi kuyamudu, kwa hivyo ikiwa sisi Wawakilishi pamoja na jamii hatujakaa pamoja tukasisitiza suala hili. Kwa hivyo, kesi za aina hii mara zote hazitakwenda mahakamani.

Mhe. Salma Moh'd Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize. Kwa kuwa kuna uzoefu unaojulikana wazee wa mtoto aliyenyanaswa kijinsia kuwa na makubaliano ya nje ya mahakama na wazee wa mtoto aliyenyanaswa.

Je, ni nini kauli ya serikali kuhusu utaratibu huo, unazidisha kasi ya unyanyasaji au unapunguza. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwa utaratibu huu unaokwenda wa jamii kesi za unyanyasaji zitaendelea kwa sababu mtu anajua baada ya kumbaka mtoto sasa mzee kwa sababu wanakaa

jirani, basi watakwenda na kusuluhishana au polisi wataingia na kuoreshana. Kwa hivyo, kile kitendo hasa hatutaweza kukidhibiti na kuwatia adabu au adhabu wanaohusika.

Sasa wito wangu ni kwamba wazee waondokane na tabia hiyo kama mtu amekamatwa amefanya vitendo hivi, kwa hiyo huu ujamaa jamaa tuondoe na tukiuongoa ujamaa tukiondoa jamii kwamba wanamsema vibaya kwamba ushahidi Mahakamani ikadhibiti wakatiwa adhabu kubwa mimi nafikiri baada ya kesi mbili tatu matatizo haya yanaweza yakaanza kupungua.

Kwa hivyo, mimi naomba kwa kutumia nafasi hii niombe jamii kwamba pale wanapoitwa kuwa mashahidi wa vitendo kama hivi wakubali na wasikatae, na wala wasisuluhishe nje ya mahakama, kwa sababu itapunguza ile kasi ya kudhibiti vitendo hivi. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kutokana na mtiririko wa kesi hizi huwa mara nyingi zinasababishwa na matokeo ambayo kesi hizi zinakuwa hazina suluhu nzuri. Je, Mhe. Waziri unaishauri nini serikali hasa kwa kuzingatia kwamba kesi hizi hazibebwi na Jamhuri.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, sisi kama serikali tumejaribu kufanya mambo kadhaa.

Kwanza kama nilivyosema mwanzo tumewaita wadau wote wanaohusiana na mambo haya wakiwemo Polisi, Waendesha Mashtaka, Mahakimu, Watu wa Afya na tukaendeleza hata hili suala la *One Stop Centre*, yaani mtoto au mtu yeyote akifanyiwa vitendo hivi basi pale pale anakwenda kupimwa na kufanywa mambo yote kwa ajili ya kupata ushahidi.

Pili hivi sasa tuko kwenye harakati za kufungua *social cases* kwa ajili hii, maana yake ni zile kesi ambazo zinasikilizwa moja kwa moja, yaani ikianza leo haisimami mpaka kesi ile kumaliza. Kwa hivyo, tutajaribu kuweka mahakimu maalum ambao watasikiliza kesi wakati wa kuanza mpaka itakapomaliza, ili kupunguza ule wakati wa kesi kwamba njoo baada ya mwezi mmoja au miwili, lakini kama ikianza leo basi inakwenda moja kwa moja mpaka kumaliza, kwa hiyo hii inaweza kusaidia.

Lakini zaidi ni kujaribu kuwasomesha au kuwaelimisha jamii, kwamba hili ni janga au ni tatizo kubwa la taifa. Kwa hiyo, jamii hasa wakiwemo wazee wa

wahusika nao wanao mchango mkubwa katika kusaidia harakati hizi za kukomesha vitendo hivi.

Nam. 57

Utaratibu wa Kuviwezesha Vikundi vya Ushirika

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa lengo la serikali yetu kupitia Mpango wa Kupunguza Umaskini Zanzibar MKUZA I – II, ni kuongezea kipato na kupunguza umaskini kwa wananchi wake.

Kwa kuwa katika jimbo la Wawi wananchi wengi wakiwemo akinamama na vijana wamejikusanya pamoja na kujishughulisha katika miradi mbali mbali ikiwemo ya uhifadhi wa mazingira (*Vitongoji Enviroment Conservation Assosiation*) VECA, ufugaji nyuki, ubanjaji kokoto, kilimo cha mboga mboga katika mabonde ya Biyani na Kogile na kwa kuwa vyote hivyo bado havijawezeshwa na wizara yako.

Je, watumie utaratibu gani, ili na wao waweze kunufaika na mifuko ya wizara yako

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 kama hivi ifuatavyo:-

Ili kuweza kunufaika na Mifuko ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, wananchi wa Jimbo la Wawi na majimbo mengine ya Kisiwani Pemba wanatakiwa kupeleka maombi yao ya mikopo katika Afisi ya Idara ya Mikopo iliyopo Madungu, Chake Chake Pemba.

Baada ya kupokelewa barua yao ya maombi, waombaji watapatiwa fomu za kuombea mikopo ambazo pamoja na mambo mengine, zinadadisi shughuli zinazoombewa mkopo, vifaa vinavyohitajika na jumla ya mkopo unaohitajika.

Baada ya waombaji kujaza fomu hiyo kwa ukamilifu, wataiwakilisha kwa Sheha wa Shehia yao kwa utambuzi, na baadaye kuwasilisha katika Afisi ya Mfuko ikiwa imejazwa kwa ukamilifu.

Baada ya fomu ya maombi kupokelewa ikiwa imejazwa kikamilifu, Maafisa wa Mfuko watawafuata waombaji kuthibitisha ukamilifu na usahihi wa taarifa zilizotolewa na kujiridhisha juu ya uwezekano wa kufanikiwa mradi ulioombewa mkopo, na uwezo wa mradi kuweza kurudisha mkopo ulioombwa.

Inapoonekana kuwa mradi ulioombwa una tija na unaweza kuwapatia faida waombaji. Mkataba baina ya waombaji na Mfuko unatayarishwa na mkopo unaotolewa.

Wananchi wa Jimbo la Wawi wanauelewa utaratibu huu, kwani baadhi yao wameomba na wamepatiwa Mikopo ya Mfuko wa Wizara.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana Mhe. Waziri ambaye ni mwalimu wangu naomba niulize swali dogo tu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wabanjaji kokoto katika eneo langu la Vitongoji kule kuna vikundi vingi tena kutoka vijijini. Vile vile kwa kuwa mfuko au mikopo inayopatikana kwenye wizara yake imekuwa na urasimu mkubwa sana kiasi ambacho watu wanaotoka vijijini kama vile mimi na wale wapiga kura wangu kule inakuwa ni tabu sana kuupata.

Je, Mhe. Waziri ni lini mtapunguza urasimu, ili na sisi washamba kule Vitongoji, Kibokoni Kisiwani, Umangani pamoja na Uwandani tuweze kunufaika na mikopo hii.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwanza nakiri baadhi ya Maafisa wetu wa Ushirika wamekuwa na urasimu mkubwa, lakini si hivyo tu kumekuwa na tatizo hata kile kiwango ambacho tumeweka basi huwa kinapangwa kwa mujibu wanavyohisi wao.

Sasa tatizo hilo husababisha baadhi ya wananchi kupata usumbufu kwa kutajiwa kiwango ambacho ni zaidi hivyo. Kutokana na hali hiyo, tumeanza kuchukua hatua na wale wahusika tumewachukulia hatua juu ya masuala hayo.

Kwa hivyo, napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba mara tutakapomaliza kusoma bajeti yetu safari hii tunatarajia utaratibu wetu wa mfuko sasa tutakuwa na mfuko mmoja mkubwa, ambao utapunguza urasimu huo hata kwa kupitia katika maeneo mengine ambayo si ya lazima, utakuwa na mkataba kati ya waombaji na wizara moja kwa moja ambayo itasaidia kupunguza urasimu huo. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe *Inshallah*

akae mkao wa kupunguza umaskini na juhudi zitafanyika, ili kuwakwamua wananchi wa Wawi na wananchi wote wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, ili wananchi wapate hiyo mikopo, basi ni budi kwanza hizo fedha za kutoa mikopo ziwepo. Vile vile nakumbuka serikali ya Kenya iliyopo madarakani sasa kupitia *Manifesto* ya *Jubilee* walitenga kama bilioni 60 za Kenya ambazo ni sawa na trilioni moja za kitanzania.

Je, serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika katika bajeti ya mwaka huu imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kuvinufaisha vikundi ikiwa ni pamoja na vijana.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwanza napenda nimhakikishie kwamba Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, wanazo fedha kwa ajili ya kuwakopesha wananchi katika shughuli zao mbali mbali. Vile vile kwenye bajeti yangu ya safari hii serikali imetenga bilioni 1.1 kwa ajili ya kuwasaidia wananchi hasa vijana katika masuala yao mbali mbali ambayo yanayohusiana na mambo ya kujiimarisha kiuchumi, pia Mhe. Rais alianzisha Mfuko wa Uwezeshaji na tunatarajia *group* la 4 tarehe 8 litamaliza.

Mhe. Spika, *Inshallah* tunatarajia kwenye Agosti 21 au 22 basi Mhe. Rais atauzindua mfuko huo, ambapo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote, Wabunge pamoja na viongozi mbali mbali wataalikwa kwenye uzinduzi huo, ili wajue kwamba fedha zile zina madhumuni ya kuwafikia hao wananchi ambao wamelengwa. Kwa hivyo, tuwe na subra kidogo na siwezi kuzitaja isipokuwa ni fedha za kutosha.

Pamoja na hayo, natarajia Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wakati atakapofanya majumuisho yake atatoa taarifa nzuri juu ya hatua ilifikiwa kuhusu fedha zile za Mfuko wa AK na JK na jinsi utaratibu utakaotumika katika suala zima la kuwapatia huduma hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Kwa kuwa wizara yake imechukua jitihada kubwa ya kuweza kutoa mikopo hii ya AK na JK kwa ajili ya kuwajengea uwezo wananchi wa Zanzibar na kuondokana na umaskini.

- (a) Je, kuna utaratibu gani ambao kuwa wizara yake inafanya katika kuona kwamba wanaochukua mkopo ule hawarejei tena.

(b) Kuna utaratibu gani wa kupima uwezesaji huo unaotolewa kuonekana mafanikio gani yanayopatikana.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba lile swali la (b) arejee.

Mhe. Spika: Mhe. Bikame Yussuf Hamad, rudia swali la (b).

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, ahsante swali (b) ni kuwa kuna utaratibu gani wa wizara yake katika kupima uwezesaji huu unaotolewa wa mikopo kuwa unaonekana na mafanikio.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwa kweli Mifuko ya AK na JK wakati ilipotolewa mikopo ile ilitolewa, lakini kwa bahati mbaya taaluma haikuwafika vizuri wananchi wenyewe, kwa maana hiyo tija haikupatikana kama ilivyokusudiwa huo ndio ukweli wenyewe.

Lakini pia tatizo jengine ni kwamba wananchi wenyewe sasa ambao wale walioelewa kwamba mikopo hii inatolewa kwa madhumuni fulani, basi hawakuamini kwamba mikopo ile imetolewa kama ni njia ambayo baadaye inahitajika kuja kulipwa. Matokeo yake wakafanya kama walivyohisi wao inafaa, wengine wameongeza majiko, wamefanya mambo mengine nje ya utaratibu.

Fedha zile kwa karibu mwaka mmoja na nusu hivi sasa hazijatolewa kwa wakopaji wanya kutokana na Benki ya Watu wa Zanzibar kuwa na mzigo huo mzito na walishindwa kufuatilia suala lile, kwa sababu ni hasara kufuatilia shilingi 50,000/= au 100,000/= katika maeneo mbali mbali na hatimaye ndipo pale wizara ilipochukua jukumu hivi sasa la kuiomba rasmi serikali ili mfuko ule upatiwe wizara yetu.

Kuhusu suala la urasimu kama nilivyozungumza kwa Mhe. Saleh Nassor Juma kwamba ulikuwepo, matatizo pia yalikuwepo na tija ilikuwa ni ndogo iliyopatikana kuliko faida iliyopatikana, isipokuwa wapo wachache ambao wamefanya vizuri. Lakini mikopo ile imezuilika hivi sasa hadi hapo serikali itatoa ufafanuzi zaidi ambapo tunatarajia katika bajeti ijayo tutaweka maelekezo, ufafanuzi na tutatoa mafunzo na tunaendelea kutoa mafunzo kwa wananchi wetu, ili tuhakikishe wanapopata mikopo ile iwe inaleta tija na maslahi yao na wananchi kwa jumla. (*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nimearifiwa kwamba kuna wachangiaji watatu wanayo mazungumzo ambayo si marefu kwa sababu hawatapenda kurejea, lakini ameongezeka na mmoja kwa niaba ya wizara na yeye anataka kumsaidia Mhe. Waziri. Kwa hiyo, tutaribu kuzungumza kwa kifupi, ili Mhe. Waziri baadaye tumuombe atupe ufafanuzi. Sasa tuanze kwa kumsikiliza Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, ambapo Mhe. Naibu Waziri wa Afya anajitayarisha pamoja na Mhe. Mussa Ali Hassan. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, kabla ya yote hayo niseme kwanza, waswahili wamesema "*ng'ombe tangulizi ndiye anakunywa maji mema*". Kwa hiyo wenzangu wengi Mhe. Spika, wameshatangulia sana kwa kuizungumzia hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa vile na miye nitakuwa na mchango kidogo ili nisipoteze muda wako.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kutuletea hotuba hii na kuweza kuichangia tokea juzi na hii leo. Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi nitakuwa nje ya kitabu hichi kinachosema hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Nianze na Fedha Mhe. Spika, Waswahili wengi husema kwamba "*Fedha ishi maana*" kwa hiyo na mimi naungana na hao waswahili wanaosema kwamba *Fedha ishi maana*. Mhe. Spika kama fedha hatuna uchumi, na kama hatuna uchumi hatuna maendeleo, na ikiwa hakuna maendeleo pia hakuna na mapato pia, nitasema hivyo. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri aungane mie kuhusu suala hili ili kuziwezesha wizara kufanya kazi zao vizuri na kuweka mipango iliyo mizuri.

Mhe. Spika, nije katika kilimo. Kilimo kama walivyozungumzia wenzangu wengi na mimi nasema sitokuwa na mengi nitazungumzia kidogo tu. Nimuombe Mhe. Waziri kwamba serikali iwawezeshe wakulima wetu kuwapatia zana za kilimo ili kuepukana na kilimo cha kutumia mikono.

Mhe. Spika, nije katika uvuvi, juzi hapa nilisikia suala ambalo linasema bahari kuu inanyemelewa na magaidi. Nimuombe Mhe. Waziri ili awawezeshe wavuvi wetu kupata zana kamili ili wanapotokewa na matatizo kama haya watu wale waweze kujihami, kwa sababu tunao wavuvi wetu wengi ambao hutembelea sehemu za bahari kuu na huvua katika sehemu hizo.

Vile vile nije katika masuala ya Mtambuka ukurasa wa 32 pia niombe serikali ichukue hatua za hali ya juu ili kuwaelimisha wananchi maana ya mabadiliko ya hewa ukaa na mabadiliko ya tabia nchi. Watu wetu wengi hawaelewi nini maana ya hewa ukaa na nini maana ya mabadiliko ya tabia nchi. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri hili alichukulie hatua za hali ya juu ili kuwaelimisha wananchi wetu waelewe masuala kama haya au maneno kama haya yanayokuja kijuu juu, kwa sababu wengi hawafahamu. Nimwambie Mhe. Waziri hili alichukulie hatua za makusudi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo kama nilivyosema nisipoteze muda wako na watu wengi tayari wameshaichangia hotuba hii na mengi ndiyo hayo hayo yanayochangiwa naomba uniruhusu nika. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii kusimama kuchangia bajeti yetu ya serikali.

Pia napenda kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kutoa mchango wangu. Pia napenda niipongeze serikali pamoja na Rais wetu kuipa Afya kipaumbele, namshukuru sana.

Pia napenda nimshukuru Waziri kwa kututengea fungu ambalo kama kweli tutapewa mambo hayatokuwa mabaya, tunashukuru kwa hilo.

Mhe. Spika, nimesikia watu wengi hapa wanalalamika utaratibu wa bajeti. Bajeti zetu Zanzibar zinategemea mambo mawili makubwa kutokana na uchumi wetu, utalii na karafuu. Hali ya Arusha mimi hainipi matumaini kwamba utalii wa hapa kwetu utapona. Umekuja Uamsho tu siku mbili tatu mpaka leo hapa hatuja *recover*, watalii wanapokuja kwa *package* ya kupitia Arusha halafu kuja Zanzibar, wakiwa hawaendi Arusha na Zanzibar hawaji. Kwa hivyo utalii si kitu ambacho sasa hivi kina matumaini makubwa kwa bajeti yetu.

Mhe. Spika, kitu cha pili ambacho tunakitegemea hapa ili hayo yaweze kupatikana amani na utulivu lazima viwepo, bila ya hivyo hakuna jinsi kwa sisi tunaotegemea amani katika maisha yetu ya uchumi.

Mhe. Spika, kwa kweli nikiangalia bajeti yetu hii nahisi kwamba yale yaliyopendekezwa ingawa wengi wanalalamikia wanasema tunakamuliwa. Kama kweli utalii hautofanya kazi, kama kweli karafuu zinategemea huko kwenye soko, leo wanataka wanapandisha, kesho wanashusha, mimi nafikiri itabidi kama nchi tufunge mkanda na hayo yaliyopendekezwa tuyakubali kwa sababu hiyo ndiyo njia pekee. Tunasema hapa tunatakiwa tujitegemee tusitegemee wafadhili, halafu tena tunasema sisi tusitozwe kodi. Sasa zipatikane wapi? Mimi ningependa wale wanaotoa ushauri huo unapomwambia mwenzio hili baya basi mwambie na zuri lipi, ili afanye. Kwa hivyo wampe ushauri mwengine Mhe. Waziri ili aweze kutafuta utaratibu mzuri wa kukusanya mapato.

Mhe. Spika, sasa niende kwa upande wa afya. Kama kweli tunataka taifa liendelee na uchumi ukuwe, nafikiri vipaumbele vilivyotolewa si vibaya. Elimu kwa wataalamu tunaowataka, afya, siha, kujikinga na maradhi ili tuweze kuzalisha, Ajira kwa vijana ndio nguvu kazi yenyewe. Maji safi na salama ni muhimu kuinga maradhi na miundombinu mbali mbali iliyotajwa nafikiri huo ni msingi mzuri. Na hivi si vitu vya kutekelezwa kwa mwaka mmoja tu, vinahitaji fedha nyingi. Kwa hivyo nafikiri kama tutakwenda katika njia hii mimi naiona kwamba ndio sahihi.

Mhe. Spika, Wizara yetu ya Afya inatekeleza dira ya maendeleo ya mwaka 2020, MKUZA II na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala CCM ya mwaka 2010. Kutekeleza hayo afya imejitapanga kwa mambo mawili kama kawaida kinga na tiba. Kinga, hapa leo nilikuwa nataka nitoe wito maalum kwa Waheshimiwa Wawakilishi, tunachangia damu jamani kwa watu wetu sijawaona Wawakilishi nataka nilete gari hapa, Wawakilishi mchangie damu, kama mtaniruhusu nitafanya utaratibu huo, hiyo ni kinga ya vifo vya akina mama na mtoto.

Elimu ya afya, redio zinajitahidi, TV zinajitahidi, kila eneo redio nyingi zinafika, siku hizi Zenji FM inafika kila pahala na huko nako tunaitumia. Lakini kitu chengine muhimu jamani ni kupima afya, tusingoje mpaka mtu unaugua tena ndio unakwenda hospitali, unatakiwa angalau mwaka mara moja upime afya yako. Naomba wananchi na Wawakilishi tupimeni afya zetu. Lakini hata hivyo kama nilivyosema asubuhi tubadilisha utaratibu wa maisha yetu ya kuishi, kula na kufanya mazoezi. Bila ya hivyo hiyo kinga tunayoizungumzia itakuwa mthani.

Mhe. Spika, mimi nimeipenda bajeti yetu hii, kwa sababu imezingatia tatizo moja kubwa la rasilimali watu. Rasilimali watu kwa Wizara ya Afya ni mthani, lakini Wizara imekubali na serikali yetu imekubali pindipo tu

tutakapopata mtaalamu wa afya tuweze kumuajiri wakati wowote. Kwa hiyo naishukuru serikali na Wizara ya Fedha kututengea fungu hilo.

Mhe. Spika, kuna jambo moja jana lilizungumzwa kuhusu wastaafu. Wizara ya Afya ni katika Wizara ambazo zinawaajiri wastaafu. Daktari hastaafu, anaweza akaacha kazi kwa tatizo maalum, hata daktari akiwa kizee ndio anakuwa anazidi kuwa na maarifa. Kwa hiyo kama kuna upungufu wa madaktari Wizara ya Afya muiruhusu iajiri hao. Jamani mtaalamu wa afya kumtengeneza inachukua muda. Kama mmeona tumepita huko na kwenye ziara kila tunapopita daktari mstaafu turudishiye daktari wetu, turudishiye daktari wetu, kwa sababu kusomesha kunachukua muda mrefu. Hilo mimi nalionga la umuhimu kwa upande wa afya ili watu waweze kuajiriwa wakasaidie watu mpaka pale mambo yatakapokaa sawa.

Mhe. Spika, pia jukumu limechukuliwa na Wizara ya Elimu SUZA itafungua Chuo cha Afya Kitivo cha Tiba kitakachosomesha madaktari. Kwa hivyo ni mategemeo yetu kwamba Wizara ya Fedha itaitilia fedha za ruzuku ili hilo nalo lifanyike tuondokane na hiyo changamoto.

Mimi ningependa kidogo nimwambie Mhe. Bikame jana kanifurahisha sana kwa maswali yake. Mhe. Bikame bwana kauliza maswali hapa mimi mwenyewe nikawa nimelala. Hata hivyo nilikuwa nataka nimwambie ndugu yangu kweli wafanyakazi wanakuwa hawapo vituoni, wafanyakazi wenyewe kidogo. Lakini kinachojitokeza kule ni mfanyakazi mara kila siku ya kuwa mapya, wafanyakazi wanahitaji kuelimishwa, kwa hiyo huwa wanatoka pale wanakwenda kusoma. Kama kituo kinamfanya kazi mmoja inabidi kibaki kitupu, lakini hata hivyo kuelimishwa ni haki ya kila mfanyakazi kwa hivyo tusiwanyime haki yao ya msingi. Lakini hata hivyo na mwananchi kupata huduma ni suala lake pia la msingi kwa sababu ni haki yake. Jana jana baada ya kulisema tu nimewatumia watu *message*, nimekaa kikao, tukafanya utaratibu kuhakikisha kwamba hilo nalo linapungua kwa kiasi kikubwa. Halafu tena msemi serikali si sikivu, tunasikia hivyo na tunayachukulia hatua.

Mhe. Spika, kitu chengine ambacho ningependa kukizungumzia hapa ni kuhusiana na Wizara kuchangia miradi. Wizara ya Fedha inatoa fedha nyingi kwa Wizara ya Afya kufanya miradi. Sasa hivi wafadhili wakileta mradi wowote serikalini wanasema ni *fifty- fifty*, tunajiandaa kwenye Wizara kwa hiyo Wizara ya Fedha inahakikisha inatia mkataba na inalichukua hilo jukumu hata kama ni mabilioni.

Wizara safari hii ina majukumu makubwa mengi ambayo itatakiwa Wizara ya Fedha ilipe pesa, kuna suala la kukuza Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya Rufaa. Kuna Mradi wa ORIO una mapesa mengi ni *fifty- fifty*. Kuna ghala ya

madawa watu wanataka ijengwe Pemba ni *fifty -fifty* na yote hayo yanataka kufanyika mwaka huu. Jengo la maradhi ya uti wa mgongo, huduma za maradhi ya mafigo. Kwa hiyo hivyo vyote vinahitaji fedha na nafikiri Wizara ya Fedha itatoa fedha nyingi kwa Wizara ya Afya kwa sababu hiyo. Kwa sababu hizo ndizo huduma tunazozitaka.

Mhe. Spika, kuna Hospitali ya Abdalla Mzee inatakiwa kujengwa iwe ya Rufaa kwa ajili ya Pemba itakuwa na kila kitu, kuna majengo pale, kuna miundombinu, kuna maji. Inabidi Wizara ya Fedha ilipe pesa nyingi kwa ajili. Mimi nafikiri Wizara ya Fedha au Wizara ya Afya kupewa kipaumbele hatukupendelewa ni kwa faida yetu sote.

Mhe. Mwanaidi jana alizungumzia nikamsikia anasemea kuhusu suala la *incinerator*. Mhe. Mwanaidi tumekusikia na tumepata fungu la fedha ambalo limetoka huko huko Wizara ya Fedha wanaliita la misamaha ya kodi, *incinerator* mwaka huu itanunuliwa.

Lakini pia tumezungumzia hapa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa alizungumzia mabadiliko ya mwendo wa maradhi, yeye akazungumzia kuhusu kisukari. Mhe. Spika, nilikuwa nataka niseme hili makusudi kwa sababu hapa nyuma kidogo limeleta mzozo na vyombo vya habari. Siku zote nitasema ikiwa havikutendea haki nitasema kwa sababu kwa hili hawakututendea haki. Hawakuja Wizarani wakauliza, wakatafuta ukweli, wanaandika habari zao kwa *hear say*, si vizuri. Kama kuna tatizo waje watuulize, tumesikia upande huu, tunataka tusikie na upande wenu ili wachanganye zile habari zilete ukweli.

Mhe. Spika, nchi inayoendelea maradhi kama hayo ya kisukari yanakuwepo kwa sababu hiyo ni dalili moja ya maendeleo. Nimesema hapa tulikuwa tunakwenda kwa miguu, sasa sote tunapanda magari. Sasa huduma za maradhi hayo huwa yapo katika utaratibu wa kinga na tiba. Kinga nimeieleza, lakini linapokuja suala la tiba kuna vidonge na sindano. Hapa nataka nizungumzie suala lililozungumzwa sana la *insulin* mpaka kwenye vyombo vya habari.

Mhe. Spika, dawa za *insulin* ambazo zilizoletwa zilizopatikana baada ya *tender* zilikuwa zinatoka India na shirika hilo au kiwanda hicho kinatoa dawa ambazo zinatumika kote Afrika Mashariki, Uganda, Kenya na hapa Tanzania madaktari wanazitumia na ukienda kwenye *pharmacy* utazikuta. Sisi tunapotoa *tender* kile tunachokipata madhali tuna hakika kwamba hiki hakina tatizo, kwa hiyo hicho ndicho tutakachokinunua, kwa sababu ndio utaratibu wa manunuzi ya serikali. Hatuwezi kusema kwamba hatununuzi kwa sababu hatulikuta Shirika hili. Sasa hao kama TSBI imekubali, ZFBE imethibitisha,

Afrika Mashariki wote wanatumia. Mimi naona hapa labda kuna maslahi binafsi ninavyohisi mimi, kwa sababu silioni jenginelo.

Mimi nataka kuwatoa hofu wananchi, dawa zilizopo tumieni hakuna serikali inayotaka kuuu watu wake, tunakuhitajini, tunataka mtupigie kura, turudi madarakani, kweli tutaua? Hatuwezi kufanya hivyo. Wale wanaona kwamba bado wanataka kumsikiliza huyo anayewashauri *pharmacy* zipo wana uwezo wakanunue, zote za aina mbili zipo, hakuna tatizo. Lakini wale masikini za Mungu ndio mtihani.

Mhe. Spika, kuna suala la Mhe. Mahmoud Muhammed alizungumzia kuhusu pesa za madawa na pesa za *global fund* kwa ajili ya mradi wa kifua kikuu, ukoma na ukimwi. Pesa za *global fund* zimeandikiwa *specifically* kwa dawa za kifua kikuu na ukimwi. Kwa hiyo hatuwezi tukasema kwamba pesa hizo tupunguziwe pesa za madawa eti kwa sababu kuna pesa za *global fund*.

Pesa ambazo wizara inatoa au wizara itapewa na Wizara ya Fedha ni kwa ajili ya zile tunazojiita (*essential drugs*); dawa ambazo zinasambazwa kwenye vituo na dawa ambazo ziko hospitalini. Pia hizo hizo ndizo zile ambazo zitakazotuletea uwezo wa kuweza kuwazalisha kina mama bure. Tumepata changamoto kubwa kipindi kilichopita kwa sababu hatukuwa na taarifa za kutosha, kina mama baada ya kusikia bure wamekuja mpaka tukazidiwa, sasa tunajipanga. Kwa hiyo hizo pesa tunazihitaji kwa ajili ya kazi hiyo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa kazungumzia suala la malaria. Mimi nataka nimwambie kwamba malaria ni kweli kiwango sasa hivi kimepanda, lakini kuna sababu. Redio na TV zinaeleza, kuna ujumbe mpaka kwenye simu siku hizi ikifika saa 4:00, fungua chandarua jifunike. Tatizo liliopo sehemu hata zile zilizokuwa malaria hayapo sasa hivi yanajitokeza. Kwa mfano Jambiani ukanda wa pwani kule wale ndio wameanza mwanzo kuanza kuyatoa malaria kule. Lakini sasa yanarudi, Jambiani, Paje, Bwejuu, Kati Bambi, Magharibi huku upande wa namba 7, Kombeni, Fumba, Pemba, Finya, mradi malaria yamepanda lakini sio kwa kiwango cha kutisha na tumeweza kuyadhibiti. Sababu kubwa zilizofanya hivyo ni mvua. Siku za mvua siku zote malaria yanakuja juu, lakini safari hii kasi imezidi.

Lakini kingine kikubwa kwamba watu wameacha kujifunika vyandarua walivyopewa. Vyandarua vimetiwa dawa wamekaa sasa hivi hawajifuniki, utafiti umefanyika. Vyandarua vimetolewa laki tano kwenye nyumba laki mbili, lakini sasa hivi zaidi ya asilimia 50 watu hawajifuniki vyandarua, halafu wanauliza malaria yanarudi vipi. Jamani vyandarua vitumieni ndio kinga ya malaria, mbali na dawa za kupuliza, chandarua ndio kinga yangu naomba mvitumie.

Kabla sijamaliza Mhe. Spika, nilikuwa nataka kusema neno moja hapa jana watu wamezungumza kuhusu rasimu. Mimi siku zote nasema suala la rasimu ya Katiba kwa nini tuyazungumze wakati huu wa bajeti. Hapa juzi tumefundishwa, semeni hivi, semeni kile, leo tunarudi kule kule. Kuna nafasi zijazwe tatu Baraza lipo, Mabunge ya Katiba yapo, kura ya maoni ipo, beni inalia huko zumari sisi huku tunaanza kucheza, hebu tsubiri isogee tufunge vibwebwe, tucheze. (*Makofi*)

Mwisho kabisa kwa shukrani zangu zote nimshukuru Mhe. Mgeni, Mwenyekiti wetu wa UWAWAZA kajitahidi kuwafundisha wanawake. Nimeona michango mingi ya wanawake tena iliyokuwa ya maana. Hapa kwa kweli anapaswa kupongezwa. Bi Mgeni, endelea mwenyewivu muache ajinyonge, tuendele mbele na kazi. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii. Vile vile sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kufika sehemu yetu ya kutunga sheria na tukawa salama na tukaendelea na shughuli zetu kwa usalama hadi hivi sasa.

Pia nimshukuru Waziri wa Fedha na watendaji wake kwa bajeti nzuri ambayo ametufikishia hapa Barazani na kuipitisha katika hali nzuri ama kuihakikisha kwamba imepangika au haikupangika.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi sana kwa sababu wenzangu wengi wameshachangia bajeti hii, na kila mmoja ameshatoa mawazo yake ambayo inawezekana tukaichangia bajeti hii ikabadilika na kuweza kuleta maendeleo mazuri kwa wananchi wetu pamoja na sisi wenyewe katika mwaka huu wa 2013/2014. Kwanza niseme bajeti hii kwa kweli ni nzuri sana, lakini kila ninavyoisoma naikuta imeumiza sana wananchi wa hali ya chini, kwa kweli haikuwasaidia zaidi bajeti hii imeisaidia serikali. Sisi ingawa tunaona tunaisaidia serikali lakini hatuisaidii serikali isipokuwa tunasaidia kundi la wanyonyaji ambao ni wezi wa serikali.

Kwa kweli tumepandisha vitu vingi sana kwa wananchi wa hali ya chini, lakini utakuta tumeisaidia serikali lakini hayo mapato yote serikalini ukienda huyaoni wala hayafanyi kazi zake inavyotakiwa. Mimi nimefuatilia sana katika kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ukurasa wa 8 nimekuta mwenendo wa uchumi wa Zanzibar kifungu cha 12. Kifungu hichi kinajali sana hali ya mwenendo wa uchumi wa hali ya Zanzibar. Lakini uchumi badala ya kwenda juu kila siku unashuka chini. Ukitizama kwamba imesaidia sana serikali kupandisha ushuru wa

mambo yake. Ushuru ule ni ushuru ambao hauwasaidii wananchi kwa sababu utaona mwaka jana na mwaka huu bajeti yake ndio ile ile katika matumizi.

Mhe. Spika, utakuta ZRB ndio mategemeo makubwa sana kuweza kupata maendeleo ya nchi yetu, lakini utakuta mapandisho yake yamekuwa makubwa sana, utakuta hivi sasa ushuru ambao umepandishwa katika *road licenses* kwa mfanyakazi wa chini tumemuuua kabisa sio kuwa tumemuumiza. Mfanyakazi wa chini hivi sasa Rais wetu ametuwekea mpango mzuri sana kwamba wananchi wote wakopeshwe vespa uwezo wa kununua vespa na baskeli hawana. Tumewakopesha vespa lakini katika kupandishwa vespa zile ushuru umetoka kutoka shilingi ishirini na nne elfu hadi shilingi sabini elfu.

Mhe. Spika, ukitizama kutoka shilingi ishirini na nne elfu hadi shilingi sabini elfu analipa ushuru. Sasa Mhe. Spika, ukitizama kutoka 22 hadi 70 hiyo kupanda kiasi gani, angalau 24 iwe robo yake au nusu yake 25 useme mwanzo ije 50, ije 60, ije 70 lakini kutoka 24 hadi 70 mfanyakazi wa chini tumemuumiza kabisa. Tukiangalia mshahara ambao tunamlipa mfanyakazi wa chini hauzidi kwenye shilingi laki moja na hamsini, sasa atakapotoa shilingi sabini elfu ambayo amekopa vespa atatoa kwenye kulipa *road licenses* Sh 70,000/- katika Sh. 150,000/- zimebaki ngapi. Ukitoka katika hizo mtu huyo anataka kula mapembe kilo moja ya mchele ya mapembe Sh. 1,200/- kwa mwezi atakula kiasi gani. Mfanyakazi huyo huyo hizo Sh 150,000/- hiyo akiumwa anahitaji kwenda hospitali akatibiwe, mfanyakazi huyo huyo ana watoto saba, kwa siku lazima mtoto mmoja ataumwa. Pia ana wake wanne kila siku mke mmoja ataumwa. Atajikimu vipi kimaisha au tumemsaidia vipi mfanyakazi wa chini katika maisha, ingawa tumepandishia serikalini.

Mhe. Spika, ukitizama ZRB, ukitizama hayo mapato ambayo yalikuwa yaende kwa wafanyakazi wa chini walipwe angalau shilingi laki tatu kwa kutwa shilingi elfu kumi. Ni mtu gani Zanzibar anayetumia kutwa ambaye ana wake wanne shilingi elfu kumi, halafu wewe unamlipa shilingi laki moja na hamsini kwa mwezi, unamuweka wapi mtu huyo. Ukitizama mfanyakazi wa ZRB ameingia kazini miaka mitano ukimuhesabu ana nyumba 10 amepata wapi, halafu unasema anaisaidia serikali. Mhe. Waziri wa Fedha nafikiri hapo hujatengeneza chochote umechemsha.

Sielewi Mhe. Waziri kama hawa watu wa ZRB, wakishamaliza kazi zao hawaji ofisini kwangu. Mhe. Waziri nafikiri ingawa ulikusudia kuisaidia serikali lakini hapa umesaidia wezi kuiua serikali. Sababu zipo ambazo zinaonesha wazi, mfanyakazi wa ZRB ana nyumba 10 ukitizama historia yake babu yake tumecheza naye, mbali baba yake anaishi katika kibanda cha mgongo, angalau labda angelirithi kwa babu yake sio baba yake, lakini mtu yule amerithi wapi kupata nyumba 10 wakati wa miaka 5 au miaka 10, halafu

mfanyakazi wa ZRB unamuweka pale kila mwaka unamuongezea kukaa pale. Haiwi jehsi anapata uhamisho leo Songea, kesho Arusha, ZRB kuna kazi ngapi hivi sasa serikali yetu angalau kuwafanyia *rotation* angalau watu hawa wapat miaka miwili na miaka miwili aje mwengine, si hivyo watatumaliza.

Mtoto akimaliza kusoma tu anakwambia mimi nataka kazi ZRB au TRA kwa nini asitake kwenda kuwasaidia wananchi au wazee wake kwa kufanya kazi ya Hospitali, anajua hakuna kitu, dawa zenyewe hakuna za kuuza, hakuna anachopata wala hataki kwenda kufanya kazi kilimo, isipokuwa anatafuta kazi kubwa. Kwa kweli Mhe. Spika, serikali tunaiumiza na tunaiua.

Hapa Barazani watu tunaowategemea sana ndugu zetu wa *back benchers* hao ndio watendaji wa Baraza la Wawakilishi nikiwemo na mimi mwenyewe na huko nje Mhe. Spika, naomba serikali iwategemee *back benchers* sio hao wezi wa kila siku. *Back benchers* ambao wa huko nje ni wale wafanyakazi wa barabarani ambao wanachimba mtaro, wanasafisha barabara na mambo mengine ya nguvu za mwili wao. Lakini wafanyakazi wasomi ambao tunawategemea hasa sio wafanyakazi hasa ni wauaji wa serikali.

Hivi sasa serikali imetoa mpango kwamba akitaka kijana kufanya kazi anakwambia kwamba tunatangaza Chuo Kikuu, tunatangaza *form six*, hiyo imebebwa sio kuisaidia serikali, hii mimi naona imeletwa na wapinga maendeleo ya serikali. Kwa sababu inajua wazi kwamba wafanyakazi wasomi wengi wao ni watu ambao wanakuwa mrengo wa kushoto kuisaliti serikali, ili ionekane haifanyi kazi vizuri. Utakuta msomi huyu anafanya kazi *theory* lakini *practical* hajui.

Mimi mwenyewe najitangaza kwamba nilikuwa askari Mwanajeshi. Nilikuwa askari wa miguu ambaye wananita *in front*, mzinga wangu ulikuwa askari wa miguu 1445. Tulikuwa wakati huo wasomi mwaka wa 70 naingia mimi hawajaingia katika jeshi. Walikuwa watu wanapiga *range* hapa na kupiga Darajani hapigi mahesabu, anasema kwamba piga namba 10, 20, kifungu 5 unapiga pale pale Darajani au Forodhani katika jumba la Forodha. Lakini leo msomi anakaa na kitabu saa nzima mpaka maadui wanafika katika maeneo yao hajaweza kujumlisha kupiga mzinga.

Kwa hivyo, mimi niko nyuma kabisa kuwakubali wasomi, wasomi si wasomi wa kipaji, wasomi ni wasaliti wa maendeleo ya serikali. Hivi sasa naiomba serikali iendelee kuwasaidia *backbenchers* ndio watakaongoza maendeleo ya nchi hii. Kuwapeleka mbele wasomi ni kuisaliti nchi hii, kwa kweli ningelikuwa namjua mtu huyo aliyetoa hii sheria ya kusema kwamba wasomi wawe mbele *backbenchers* nyuma kwa kweli mimi ningelimshtaki katika

serikali za Umoja wa Mataifa kwamba hawa watu wanaisaliti Zanzibar. (Makofi).

Mhe. Spika, kipindi kirefu mimi nilikuwa nakwambia kwamba unanipeleka Pemba na Pemba mimi nimeshaizoea, lakini kwa kweli mara hii Mwenyezi Mungu alipoamuru umenipeleka Uganda, tarehe 6 nimekwenda Uganda. Kwa kweli katika walioibomoa Uganda mimi mwenyewe mwaka 1978. Nilipoiona Uganda ambayo niliibomoa mwaka 1978 nimekwenda mwaka 2013 nimeshangaa. Na ukweli ningekutolea picha ambayo nimepiga na Rais wa Uganda na ukweli tuliokwenda nao aliona kwamba Rais wa Uganda aligeuka kutizama aliambiwa hawa vijana kutoka Zanzibar, ni peke yetu aliyeweza kugeuka nyuma akaweza kuzungumza vizuri na sisi. Pale kulikuwa na Rwanda, kulikuwa na Burundi kulikuwa na Tanzania Bara, tulikuwa na Uganda wenyewe na Wakenya lakini sikumuona Rais Museveni kusimama lakini tulipozungumza sisi alisimama na akageuka nyuma na kutuona sisi na alifurahi sana.

Ushahidi wenzangu tuliokuwa nao wanajua, kwa kweli Uganda sasa tangu mwaka 1978 tumeibomoa ilivyojengeka aina yake utashangaa. Zanzibar ilibomolewa mwaka 1964 hadi leo Zanzibar haijajengeka popote kwa kweli Mhe. Waziri ukienda katika maeneo ya Mbweni na sehemu nyengine ukikuta hayo majumba ya mtu mmoja mmoja sio kwamba imejengwa Zanzibar amejijenga mtu utashangaa. Mimi nilitembea katika maeneo nyuma ya Chuo cha Afya nilikuwa sijaenda nyumba mpaka kwenye Mikoko ndani ya bahari tena za kifahari, nyumba zile si za serikali kwamba watakaa wananchi wao, za mtu mmoja mmoja. Wanapata wapi maendeleo haya watu wa serikali tusipate sote kwa pamoja? Mhe. Waziri naomba msaada wako kwa kweli uupangishe upya ili wananchi *back bencher* wajihakikishe kwamba wanapata maendeleo.

Maendeleo kwa kweli Mhe. Spika, hivi sasa kwa kuisaidia serikali namuona sana Rais wetu anapokwenda nje, juzi nilimuona katika hotuba yake wakati yupo China alijinata sana na kujiamini katika uvuvi wa bahari kuu. Uvuvi wa bahari kuu Zanzibar tuna bahari kubwa sana ambayo sasa hivi tunaitegemea sana hata kutuletea gesi na mambo mengine. Lakini utakuta tunasema tu bahari kuu tutatoa maendeleo hayo tutatoa kivipi bahari kuu mpaka iwe ni Zanzibar kweli. Kwa kweli Mheshimiwa bahari kuu inatakiwa viende vyombo vya kileo kuweza kuvua bahari kuu na samaki ambao wanaotakiwa mwenyewe aliwataja seneta samaki hao siwajui watamu kiasi gani ambao wanauza uzunguni tunaweza kupata pesa za kigeni. Lakini kwa ngarawa hii ya msufi au muembe hatufiki, lakini utakuta bajeti yetu imeipangia uvuvi kununua meli pamoja na kuwasomesha wananchi ili kuweza kukaa kwenye meli hii angalau watu 60 kwenye meli moja wanapewa milioni mia moja waweze kununua meli, iweze kuwasomesha, iweze kuhudumia itie mafuta na

kuweza kwenda bahari kuu. Ukweli huo ndio kweli Mhe. Waziri anaipendelea nchi hii iweze kuleta maendeleo.

Mimi naona Mhe. Waziri hapa amechemsha Wizara hii ya uvuvi kwa hakika bajeti iliyopewa iondoke kabisa na ipewe sio milioni ipewe bilioni iweze kufanya kazi za uvuvi wa bahari kuu hiyo nitaunga mkono. Sababu mimi mwenyewe niko katika Kamati hiyo ya Uvuvi, Utalii na Mifugo, ambao vitu vyote hivyo ambavyo vinafanywa na *back benchers* wa huko nje, katika sehemu hizo akiambiwa aende msomi kuvua atakwambia yeye suala hilo haliwezi. Kwa hivyo mimi naona tubadilike tuwape nafasi *back benchers* ili tuweze kusaidia serikali yetu na naamini kwa mwaka mmoja Zanzibar itabadilika na tukishirikiana na sisi *back benchers* wa barazani humu kabla hatujamaliza muda wetu wa kwenda vijijini tutawasaidia *back benchers* wa uraiani tuweze kuigeuza Zanzibar, si hivyo serikali yetu kila siku itafujwa na itatukanwa na kuona kwamba maendeleo hayapatikani kwa kusema tunawathamini wasomi.

Mhe. Spika, ukitizama hivi sasa mwalimu wa zamani ambae darasa lake la nane ama la kumi analipwa shilingi 130,000 au shilingi 150,000 mwalimu huyo ukimuuliza historia yake mimi mwenyewe nina miaka 60 na wewe Mhe. Spika, ulioko hapa ametusomesha amefanya kazi miaka 38 ya kutusaidia sisi lakini ana darasa lake la kumi, kwa vile Mhe. Spika, una *form VI* yako hapo na Chuo utasema au mimi ninalipwa milioni nakwenda nje mie nina milioni pamoja na wenzangu ambao wanajiita wasomi. Mwalimu yule tunamcheka analipwa 120,000 mpaka 150,000, kwa kweli tunamuweka wapi mwalimu yule ambaye ametusaidia sisi kutufikisha hapo ambao tunaita wasomi.

Mimi naona Mhe. Spika, watu ambao wametulea na wametusomesha kwa kweli ipangwe upya bajeti yao angalau ile nyongeza ya mwaka mmoja kupanda apandishwe angalau shilingi elfu kumi, kumi kwa mwaka angalau amkaribie huyu msomi. Atakuwaje mtu huyo ataithamini serikali na kuipenda serikali wakati ameona kwamba yeye serikali inasaliti maisha yake na familia yake. Kwa kweli watu ambao wamekuja kusema kwamba wasomi ni bora ni wasaliti wa serikali, na serikali pindi haikunyanyuka kutoa uso juu kwa kweli ielewe kwamba inapigwa vita na itaangushwa serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa kweli mimi mwenyewe ni Mwakilishi wa Chama cha Mapinduzi sitokubali kwamba chama changu kiweze kusalitiwa kwa kusema kupangiwa mambo yasiyofaa. Ninamshauri Mhe. Rais awaite Mawaziri wake wote kuhakikisha kwamba katika hiyo bango kitita ishughulikie kwanza mambo ya *back benchers* wa huko uraiani. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa kweli nimeweza kuchangia haraka haraka kuhusu hali ya serikali yetu inavyotekelezwa. Ushauri wangu hivi sasa, mimi sijafika China

lakini najua karibuni utanipeleka China kwa sababu ushaona vitu vyangu, hapo Uganda tu nimekuletea habari za Uganda nikienda China nitakuletea habari za kichina sio wengine ambao wameenda China hawatoi faida ya China wameona nini. Mimi naamini China utajiri wake haukuendesha na wasomi watupu, China uchumi wake umeendesha na askari wa jeshi la nchi ya China ndio walioendesha China kuweza kufikia hatua iliyofika leo. Unamkuta raia yoyote mtu wa Benki au sehemu nyengine hawezi kukaa Benki au TRA au ZRB kama hajakipita kwanza jeshini. Ukipita jeshini, jeshi tunaambiwa ni chuo popote. Sasa mwanajeshi yule ndiye aliyesaidia nchi ya China kuifikisha hatua waliyofika kwa sababu ninajua Mhe. Spika, wewe umeshafika kama si mara moja au mara mbili, mimi iko siku utanipeleka najua.

Kwa kweli hivi sasa tubadilike katika sehemu zetu za utalii, utalii ZRB ndiko inakotumaliza, wanakuja watalii 300 kwa siku katika hoteli moja ya kifahari iliopo Kiwengwa ambako nimelala mimi juzi, mimi na wewe tuliona hali ya watalii wanafika pale watalii 300 lakini kwa vile muendeshaji wa hoteli ile anaambiwa hapa umekuja kutafuta hukuja kusaidia watu. Tulipe watalii waliolala humu leo 200, 100 tunakuachia ahsante yako lakini hizo pesa zije huko ZRB tugawane ushahidi tunao. Wanapewa ZRB na TRA fedha zile utakuta ndio wana sababu ya kuwa na majumba kumi kumi. Ukienda hotelini unaambiwa wamefika watu 200 kumbe wamelala watu 300 pale mapato yamevuja sana. Ushauri wangu tunavyo vikosi vyetu vya ulinzi na usalama iweje ulinzi na usalama tusiwape nafasi kila siku kwenda kwenye hoteli kuhakikisha leo wanalala watu mia ngapi katika hoteli na kuzileta fedha zile katika sehemu inayotakiwa ili kurikodiwa kwa kila siku wabadilike watu sio wale wale ambao mwaka mzima anakaa anazoeana na watu wa hoteli na ndio wanapeana ushauri kuimaliza Zanzibar.

Lakini kama ulinzi na usalama kila siku tunabadilisha mtu kwenda sehemu za mapato nahakikisha kwamba Zanzibar itabadilika si zaidi ya mwaka mmoja. Lakini keshokutwa tunatimiza miaka 50 ukija kwenye bajeti pale pale unamlipa mfanyakazi 150,000 tutaenda wapi badala ya kuitukana serikali au kuisaliti. Kwa kweli kama hatujabadilika Mhe. Spika, nchi tunaipoteza na tutaipeleka sipo. Kwa sababu wizi ukiwa mwingi tunaisaliti serikali na hata serikali itakayokuja watajua kwamba tumeisaliti iliyopita vipi wao watajipanga upya, hawatochukua wasomi watachukua *back benchers*. Lakini tuanze sisi tuliokuwa madarakani sasa hivi tunyanyuke na tujue kosa letu lipo wapi wasomi ndio wanaotumaliza. Hakuna msomi aliyeko TRA akawa na nyumba 3 au nyumba 5 lakini ninakuhakikishia marehemu Mzee Karume amekufa ana nyumba yake moja pale Maisara ndio nyumba ninayoifahamu ya Marehemu Mzee Karume, nyumba moja na ndiye aliyepindua nchi hii na wenzake, ana nyumba moja iweje sisi warukia uda tuna nyumba kumi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa muda wako unamalizika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mheshimiwa naomba dakika tano. Mhe. Spika, kwa kweli leo nimezidi kusema mengi mengine ndio mengine labda wasomi watasema sio lakini Mhe. Waziri bajeti anayepanga abadilishe na sehemu anazowaweka watu katika maofisi yake achukuwe kila baada ya miezi 6 awabadilishe kuweka wengine, kwa sababu wasomi ni wengi na waliokwisha kusomea kazi ni wengi lakini hivi sasa wako *back benchers* hawana nafasi.

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa *speech* yangu ndogo lakini ni nzuri. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia bajeti hii. Mheshimiwa nikushukuru na nimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa kutuletea makadirio na mapato ya matumizi ya mwaka huu 2013/2014 na Mheshimiwa kwanza niseme naunga mkono hoja, katika michangio hapa Mheshimiwa ya Wajumbe wako kuna wawili watatu ambao wamechangia, mengi tutakuja jibu katika bajeti yetu lakini yale machache nilihisi niyatolee ufafanuzi.

Na Mhe. Spika na niseme kama tulikotoka ni mbali na tunakwenda hatujasimama, changamoto ni nyingi lakini changamoto kuna njia mbili; moja ni kuonesha njia palipo na tatizo ukaweza kulitaua. Sasa serikali yetu inajitahidi na naamini siku hadi siku mambo yataweza kubadilika na yataweza kukaa sawa, mahitaji ni mengi na uwezo wetu kifedha ni huu ambao tumeuona hapa Mhe. Waziri katuletea.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna suala zima ambalo alilizungumza Mhe. Bikame juu ya madarasa ambayo tunajenga nguvu za wananchi, na yeye akasema tunajitahidi kujenga ni kweli lakini akasema kama tuna kasoro moja tukipata kipya hatutizami cha zamani. Akasema kama kuna skuli zetu nyingi ambazo ni mbovu na zinahitaji matengenezo. Mheshimiwa ni kweli lakini sio kama tukipata kipya hatutizami cha zamani, cha zamani tunatizama na tunatengeza, kuna skuli nyingi ambazo tunatengeza, nyengine tunatengeneza kwa pesa zetu za ndani lakini nyengine tumezifanyia mradi maalum, mfano hai katika mwaka huu ambao tunamalizia tumetengeneza skuli sita Unguja na Pemba. Pemba tumetengeneza Utaani, Uweleni, Fidel Castro. Na kwa Unguja tumetengeneza Tumekuja, Hamamni na Forodhani hii ni katika mradi wa *World Bank*. Na skuli nyengine ambazo tunazitengeza kwa pesa zetu za ndani Mheshimiwa.

Lakini pia kulijitokeza suala la upungufu wa madarasa hasa katika Wilaya ya Magharibi. Mheshimiwa niseme ni kweli na hilo kama Wizara tumeliona tuna matatizo makubwa Wilaya ya Magharibi na kama sensa yetu tumeiona inazungumza sehemu hii ya Mjini Magharibi ni sehemu ambayo inahamia watu kila siku. Kwa hivyo kila ambavyo unajitahidi kujenga lakini mahitaji ya wanafunzi wetu kila mwaka yanazidi. Kila mwaka Mhe. Spika, tunajenga na kila mwaka ukienda maskulini mahitaji ni makubwa zaidi. Kwa kuliona hilo Mhe. Spika, kuanzia mwaka jana tuliweka mradi maalum ambao jumla yake ilikuwa tunahitaji kujenga karibu madarasa 32, na mpaka hivi sasa tumefanikiwa kujenga madarasa 18 katika skuli ya Kinuni, Fuoni, Birikani, Chuini na Kianga.

Pia tumejenga skuli moja hii tumepata msaada kutoka kwa ndugu zetu wa China ya Kwerekwe hapa inaitwa Skuli ya Urafiki yenye madarasa kumi na mbili ambayo itakwenda kwa mikondo miwili, kwa hivyo ni kama madarasa 24, kwa sababu wataingia asubuhi na wataingia na jioni. Na kwa mwaka huu pia tunatarajia tujenge skuli mbili katika Wilaya hii ya Magharibi ambayo itajumuisha madarasa 30 na pia tumezungumza na Balozzi kuna skuli nyengine moja ambayo atatumbea yenye madarasa kumi na mbili hivyo hivyo. Kwa hivyo tunatarajia Mhe. Spika, tatizo hili litapungua siku hadi siku.

Mhe. Spika, niliyotaka kuzungumza ni hayo tu ambayo yamegusa Wizara yetu kwa jumla na zaidi niseme kuwa naunga mkono hoja. Ninakushukuru sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru sana kupata dakika chache hizi kuchangia mawili matatu katika hotuba ya Mhe. Waziri juu ya mpango wetu wa maendeleo na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha.

Kwanza niseme nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa sana waliyoifanya. Mhe. Spika, naomba sana kusisitiza suala la kuwaamini wapangaji wetu na wataalam wetu hili ni suala la msingi sana na katika mafanikio ambayo serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar niseme tumefanikiwa ni hili moja. Takriban sekta zote sasa tuna wataalamu wetu na hawa wataalamu wana *challenge* kubwa sana, kuna wengine walikuwa *challenge* hizo hawawezi kuzivumilia wakasema aa sisi tunatafuta *green pastures* wameondoka. Lakini wengine wengi wamebaki alhamdulillah wanafanya kazi nzuri sana. Sasa naomba sana Mhe. Spika, sote kama Wajumbe lazima tujenge imani kwa wasomi wetu kwa wataalamu wetu hawa watu wanawaita ndio *think tank* hao ndio wanaobuni mipango, hawa ndio wanaoendesha nchi, kwa kusikilizana pamoja na wanasiasa na wengine.

Mhe. Spika, hivi sasa wakubwa wa ulimwengu tukisema wakubwa wa ulimwengu G8 walikuwa *London* wanakutana, wanakutana kule na wao *theme* yao walikuwa wanazungumza mambo matatu. Wanazungumza *stability*, wanazungumza *growth* na wanazungumza *jobs*. Marekani wanaita *jobs* sisi tunasema kazi au ajira. Lakini *stability* sio *stability* ya amani aa, wanazungumzia *macro economic stability* utulivu na uendeleu wa uchumi, ni *economic forum*, zaidi wanazungumzia uchumi na ukuaji wake *growth* na matatizo ya ajira. Leo ukiisoma hotuba hii vizuri ya Serikali Mheshimiwa kwa njia moja au nyengine tumeyagusa kwa undani sana haya mambo matatu yaliyozungumzwa. Tumeyazungumza vizuri sana na tumeonesha hali yetu ikoje na hali ya kilimwengu ikoje na sisi twende wapi. Kwa hivyo mimi natoa pongezi sana kwa Wizara ya Fedha mimi nasema wanatuongoza ndivyo. Na matokeo haya ya *speech* hii Mhe. Spika, sio matokeo ya Wizara ya Fedha peke yake, haya ni matokeo yetu sote kwa mwaka mzima. Yamefanya utafiti, baada kufanya utafiti wakafanya *consultation* au wakafanya mashauriano na *private sector* na sekta mbali mbali mpaka wakafikia kutunga hotuba hii na kutoa vitabu viwili hivi jumla vitatu.

Mimi nasema Mhe. Spika, tuwapongezeni sana sana na ninawaomba sana wenzangu katika bajeti zetu za mawizara tukivisoma hivi viwili pamoja na hizo hotuba nyengine zinazokuja naamini tutapata uelewa mzuri wa mambo yetu mbali ya semina tulopata. Kwa hivyo mimi Mhe. Spika, baada kuiona ile *theme* yetu sisi kama Waziri alivyoitaja ni bajeti ya huduma za jamii kwa wananchi wa Zanzibar. Ni kweli G8 leo hazungumzii huduma za jamii wao wanawaza uchumi tu, lakini sisi tunazungumzia hivi vipaumbele ambavyo Mhe. Waziri amevitaja. Maji safi na salama, sekta ya elimu, sekta ya afya, *program* ya ajira, hivi ndio vipaumbele vyetu. Nilisikia mtu akizungumza kwamba hatuna vipaumbele si kweli hivi ndio vipaumbele tumevitaja nam-*quote* Mhe. Waziri amesema kwamba maeneo haya manne yamepewa kipaumbele na yametengewa jumla ya shilingi bilioni 113.2 kati ya bilioni 305.4 au zaidi ya theluthi moja ya mpango wa maendeleo kwa mwaka huu. Hii hatua nzuri sana Mheshimiwa. Na imebidi haya tuyasimamie wenyewe kwa sababu *donors* kwenye jaduveli pale kwenye ukurasa wa 57, ukiangalia ukurasa wa 57 Mhe. Mwenyekiti utaona kwa mwaka ujao wa fedha mchango wetu wa serikali kwa miradi hii ya maendeleo tunategemea au tunakisia kutumia shilingi 70 bilioni na washirika wa maendeleo 235.4 bilioni. Kwa asilimia ni ongezeko asilimia 46.1 kwa serikali.

Lakini washirika ni *negative* yaani itapunguka kwa asilimia 19.7. Hii inaonesha wazi kwamba hawa watu kweli marafiki zetu, washirika wetu wa maendeleo lakini si wa kuwatumainia moja kwa moja lazima wenyewe tuvute soksi tujipinde kama alivyosema Waziri tuoneshe, tuzibe mianya ya kukusanya mapato yote tupate mapato, mipango yetu ya maendeleo iende.

Mhe. Spika, hili suala nimeona nilitilie mkazo ni suala la umuhimu sana. Naomba mimi nisisitize zaidi katika suala zima katika hivi vipaumbele vyetu vinne suala la usimamizi, suala la ufuatiliaji na suala la ufanyaji tathmini mimi ninaipa *three use*. Usimamizi, ufuatiliaji na ufanyaji tathmini kila tunapokwenda haya mambo tuwe tunafanya mapitio ya mara kwa mara tuone tunakwenda vipi turekebishe usingoje mpaka mwaka umekwisha ndio tunafanya *review*, ninafikiri haya yatatusaidia sana.

Mhe. Spika, nimalizie tu kwamba mbali ya vipaumbele alivyoonesha lakini Mhe. Waziri pia katika utekelezaji wa dira 2020 na Mkuza amezitaja programu tano ambazo kazigusa kwenye kitabu hiki ziko kwenye ukurasa wa 31 na 32. Nataka kusema kwamba katika vile visaidizi 5 kile cha mwisho ambacho mwenyewe kakiita *enablers* au visaidizi, visaidizi vyenyewe kama unasema uimarishaji wa miundombinu, kukuza ujuzi wa kazi na ujasiri amali. Kwa kweli haya mambo ni muhimu sana Mheshimiwa, miundombinu kwa upande wa barabara serikali yetu imefanya kazi nzuri sana, lakini tusiachie mpaka miundombinu tena ile ikaharibika. Juzi nilikwenda Mkoa wa Kaskazini nikakuta *stretch* au kipande cha barabara pale Mkokotoni kidogo siku nyingi hakijashughulikiwa, watalii wetu wanaokwenda kule tena aa wasipate vumbi. Kwa hivyo mambo kama yale yawe endelevu tusirudi nyuma. Kwa hivyo mimi Mhe. Spika, nilikuwa sina mengi nilitaka nikazie tu.

Na mwisho kabisa Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Juma alizungumza suala la Darajani na akauliza hivyo serikali haina mipango ya kudumu pahali pale. Mhe. Spika, mipango ipo, na wameshajitokeza wawekezaji wawili pale kujenga *shopping mole* pale aina moja ya uwekezaji ni wazawa wenyewe wazanzibari wenyewe wameshakuja na *plan* zao na michoro yao na njia watazopata fedha. Lakini pia kaja muwekezaji mwengine wa kigeni, na ina michoro yake na mapendekezo yake na wapi atapata fedha. Kazi hiyo Mhe. Spika, tumeichukua tumewapa wataalamu. Kama nilivyosema lazima tuwaamini wataalamu wetu, hali ya Darajani sote tunajua chimbuko lake pale kwenda kujenga nyumba ghorofa nne ufikirie msingi wake usiende ukagusa maji. Sasa tumewapa wataalamu tufikirie kama *mole* utakuja kuweka magari mengi 200 kwa mpigo, ufikirie nafasi hiyo itatosha na skuli pale. Sasa tumewakutanisha wataalamu, na nimeambiwa kwamba wakati wowote ripoti yao itatoka, wanapendekeza au hawapendekezi au tufanye vipi. Lakini serikali Mhe. Spika, pahala pale na mipango mikubwa nayo kuondosha yale mambo yanayotokezea ya kufanya biashara mahali pasipostahiki, kufurahishana hatupendi yale. Kwa hivyo tuna lengo kubwa kabisa na la muda mrefu kuweza kuwa-*accommodate* wafanyabiashara wale katika mahali pazuri.

Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii na bajeti hii kwa asilimia 100. Ninakushukuru sana kwa dakika ulizonipa. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kumuomba Mhe. Waziri kuja kufanya majumuisho ningetegemea ukumbi ujae kwa sababu tunazungumza jambo la wananchi, sasa nikiona mapengo mapengo na wananchi wenyewe hawatatufahamu. Naomba basi wale Waheshimiwa walioko nje ya ukumbi huu waingie ndani wakati Mhe. Waziri anafanya majumuisho.

Sasa ni zamu yako Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, na mimi nataka nianze pale ulipomalizia Baraza lako hili lina Wajumbe 81 lakini ndani wapo 29, tunapozungumzia *seriousness* lazima tuanze kwetu sisi Waheshimiwa. Tunapowaambia watendaji ni wezi na wananchi wakitazama humu ndani hatumo na tunalipwa na wananchi na wao watatwambia sisi tunaiibia serikali. Nazungumzia hivi kwa sababu Mhe. Spika, mimi ndio niliopewa dhamana kutafuta fedha kwa ajili ya vyombo hivi, nakuomba sana Mhe. Spika, tuwe wakali kidogo wa kuwemo ndani ya Baraza, hasa katika kipindi hichi cha bajeti ni muhimu sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nataka nianze kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kuichangia bajeti yetu hii. Lakini vile vile nataka nikushukuru wewe mwenyewe Mhe. Spika, kwa kuliongoza Baraza lako Tukufu tokea nilipoanza kusoma bajeti yetu tarehe 12/6/2013 hatimae leo hii unanipa nafasi ya kufanya majumuisho. Nakushukuru sana Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Naibu Spika, na Wenyeviti wote kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya, na nakuombeni viongozi wetu muendeleo kulisimamia Baraza letu tukufu ili tuweze kukamilisha bajeti yetu kwa salama na amani.

Mhe. Spika, kulikuja na maoni kwamba wengi walinambia kuwa katika taarifa yangu kuna taarifa ambazo hazikuwemo, mimi nilitaka kuandika kila kitu na kukisoma hapa, lakini kile nilichokiandika Mhe. Spika, au kile nilichokisoma nimetumia saa moja na dakika ishirini, nilipomaliza macho yanauma, miguu inauma, kiuno kinauma. Sasa ningeliandaa kama ile ya mwaka wa kwanza ambapo nilitumia masaa mawili na dakika kumi nadhani ningewachosha sana Waheshimiwa Wawakilishi. Lakini nilichokifanya nimeandaa vitabu vitatu, vitabu vyote hivyo vina taarifa za kutosha sana, kwa hivyo kwa Mwakilishi ambaye anataka kujisomea kufahamu ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu basi ni nafasi tosha kuweza kupitia hizo taarifa au hivyo vitabu vitatu.

Mhe. Spika, waliochangia kwa maandishi ni mmoja ni Mhe. Mlinde Mabrouk Juma. Lakini wapo ambao waliochangia kwa kuzungumza, wapo 38, naomba Mhe. Spika, kwa ruhusa yako niwatambue basi.

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali
4. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
5. Mhe. Mansoor Yussuf Himidi
6. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
7. Mhe. Fatma Mbarouk Said
8. Mhe. Ali Salum Haji
9. Mhe. Hija Hassan Hija
10. Mhe. Salmin Awadh Salmin
11. Mhe. Farida Amour Mohammed
12. Mhe. Mgeni Hassan Juma
13. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
14. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
15. Mhe. Ashura Sharif Ali
16. Mhe. Abdi Mossi Kombo
17. Mhe. Salma Moh'd Ali
18. Mhe. Asha Bakari Makame
19. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
20. Mhe. Marina Joel Thomas
21. Mhe. Mohammed Haji Khalid
22. Mhe. Saleh Nassor Juma
23. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
24. Mhe. Omar Ali Shehe
25. Mhe. Nassor Salim Ali
26. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
27. Mhe. Rufai Said Rufai
28. Mhe. Asha Abdu Haji
29. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
30. Mhe. Salum Abdalla hamad
31. Mhe. Ussi Jecha Simai
32. Mhe. Hassan Hamad Omar
33. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
34. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
35. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
36. Mhe. Mussa Ali Hassan
37. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
38. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, wachangiaji 38 wametumia dakika 810. Hoja na maoni yaliyotolewa kwa wachangiaji 38 pamoja na yule mmoja ambaye aliyehandika kwa maandishi, hoja na maoni 295. Nikisema nianze kujibu hoja 295 moja baada ya moja tutamaliza kesho. Mhe. Spika, nilichokifanya nimezi-*group* hizi hoja katika makundi na nitaomba kwa ruhusa yako na kwa idhini yako nijibu kwa pamoja kimakundi badala ya kwenda hoja moja baada ya moja.

Mhe. Spika, naomba nianze na hoja ya pato la mwananchi ni dogo. Wawakilishi wengi wamezungumzia hoja kwamba pato la mwananchi ni dogo, mwengine akiwemo Mwakilishi wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe ameielekeza na kuifanisha na maeneo mengine kama vile Qatar, ni sawa tu, ukweli utabakia pale pale kwamba pato la mwananchi wa Zanziabar bado ni dogo. Na kuna sababu za msingi Mhe. Spika, Qatar, Luxemburg mapato yao ni makubwa na wana sababu za msingi. Kwa upande wetu sekta zetu bado ni changa, tumezungumza hapa tumezungumzia sana katika sekta ya viwanda, sekta zetu bado ni changa. Lakini vile vile Mhe. Spika, hata hizo ambazo zinazofanya vizuri tunafika pahala tunazitokonyoa.

Mhe. Spika, nimetoa mfano mdogo baadhi ya Wawakilishi hapa wametoa mfano, mwaka jana tumekwenda kuichezea sekta ndogo ya Utalii tumeanzisha vurugu Zanzibar, Wazanzibari vurugu, mtalii gani atayekwenda katika pahala penye vurugu. Mimi nasema kwamba amani na kujituma ndiko kutakotusaidia Wazanzibari kuongeza mapato yetu. Lakini vile vile Mhe. Spika, mimi nimewasikiliza vizuri sana baadhi ya Wajumbe hapa, wanasema nyumba ya masikini ina watoto saba na wake wanne, kuna mtu aliyekuja akakwambia uoe wake wanne, kuna mtu aliyekuja kukwambia kwamba uzae watoto saba, ni matakwa yako na mapenzi yako. Hii nina maana gani Mhe. Spika, nina maana kwamba mzigo wetu wa wanaotutegemea yaani watoto chini ya miaka kumi na tano na wazee zaidi ya miaka 65 asilimia 47, asilimia 47 ya watu wetu wa Zanzibar hawana kazi hawawezi kufanya kazi tena, wanawategemea wale 53 na ukiwatoa hawa asilimia 47 watoe waliokuwa hawawezi kufanya kazi, chukua waliobakia halafu gawa kwa lile pato la taifa ulitazame pato la taifa litakapokuwa limeongezeka. Lakini kwa sababu taaluma inatwambia hatugawi pato la taifa kwa wanaoweza kufanya kazi tu, ndio kwa maana tukagawa kwa kila mmoja aliyepo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, ushauri wangu ninasema kwamba tujitume Wazanzibari. Ushauri wangu tutatufe, tutengeneze familia ambazo tuna uwezo nazo, kama una uwezo wa kuzaa watoto kumi zaa, kama huna uwezo wa kuzaa watoto kumi tafuta wawili wa kukutosha, ili sote kwa pamoja tunapolizungumzia pato la mwananchi angalau liwe la mwananchi. Lakini vile vile Mhe. Spika, tusichague kazi.

Mhe. Spika, nataka niunganishe hapa hapa kwenye ajira. Tumelizungumza sana kuhusu habari ya tatizo la ajira kwa vijana wetu, asilimia 17 ya waliokuwa hawana kazi ni vijana na mimi nataka niseme kwamba ukifanya by *gender* wanawake ni wengi kuliko wanaume. Somo yangu amezungumzia isitengeneze ajira itengeneze mazingira ya kuzalisha ajira, mimi nakubaliana nayo sana, Serikali jukumu lake litengeneze mazingira ya kuzalisha ajira, lakini hebu tuangalieni tumetengeneza mazingira na tumetoa kila misamaha, utalii umekuwa Zanzibar, tuna mahoteli kibao Zanzibar, Zanzibar tuna *five stars* kuliko Mkoa wowote Tanzania Bara, zaidi ya 15 tunazo *five star* Zanzibar. Lakini ukienda ukifanya uchambuzi wa mfumko wa bei utagundua katika miaka miwili iliyopita mfumko wa bei Zanzibar umesababishwa zaidi na samaki, katika kile chakula samaki ndio waliopandisha bei za vyakula. Je tumetengeneza ajira sisi kama Wawakilishi wa wananchi hebu tujiulizeni wangapi katika majimbo yetu tumetengeneza *fish farm* wangapi na tuna mahoteli tukatoa ajira kwa vijana wetu.

Kwa hivyo mazingira ya kutengeneza ajira Serikali inatengeneza, Serikali tumefungua milango kwa ajili ya *private schools* na *private hospitals*. Je, wangapi tunawahamasisha watoto wetu kusoma masomo ya sayansi, hatuna walimu wa sayansi tuna matatizo. Kwa hivyo mazingira ya ajira tunayatengeneza lakini na sisi wazazi na sisi wazee na sisi viongozi wa kisiasa tunawashajihishaje wananchi wetu, tutapiga kelele Serikali itatengeneza ajira, Serikali itafanya nini kama na sisi hatuwaoneshi wananchi wetu njia bora ya kuzitumia zile ajira zitachukuliwa na wageni, atakayefungua mradi hapa anataka wafanyakazi kama Wazanzibari hampo watakuja wengine watajaa. Nataka nikubaliane kabisa na somo yangu kwamba mazingira lazima Serikali itengeneze na Serikali itatengeneza mazingira na tutaendelea kutengeneza mazingira ili vijana wetu wachangamkie ajira.

Mhe. Spika, nikiyazungumza mazingira yapo mengi tu lakini tukifanya Kamati hapa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi halafu tuende kwenye mazingira ya kuzalisha kazi tukawatizame Wazanzibari wangapi wanaofanya kazi kule, tunaweza tukashangaa hata asilimia 20 pengine hawafiki, tunachagua kazi, tusichague kazi kama kazi ni halali tufanyeni kazi ambazo ni halali.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo imezungumziwa sana na Waheshimiwa Wajumbe ni upatikanaji wa maji safi na salama, na mimi nawashukuru sana na nawapongeza sana wale wenzangu wanaotoka katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Mkoa huu ni kitovu cha matatizo ya maji, sisi Serikalini wenzangu Waheshimiwa Mawaziri watakubaliana na mimi tumelizungumza, tumesema nguvu zetu tupeleke kutatua tatizo la maji na hasa katika Mkoa huu wa Mjini Magharibi, tatizo la maji limekuwa sugu, sio kwamba Serikali

haijaliona hili tatizo, tumeliona hili tatizo na ndio maana tumesema maji ni kipaumbele, sio kwetu sisi tu binaadamu hata kwa mimea hata kwa wanyama, huwezi ukakataa kwamba maji si kipaumbele, tumesema maji ni kipaumbele na tumetenga shilingi bilioni 46.5 kwa ajili ya usambazaji wa maji na tumetengeneza mradi maalum kwa ajili ya Mkoa wa Mjini Magharibi na tumetenga shilingi bilioni 8.8

Mhe. Spika, nimeeleza katika hotuba yangu kwamba Mawaziri hawa watakapokuwa wanakuja wataeleza mafanikio na changamoto katika kila sekta. Nawashukuru sana Dkt. Sira, namshukuruk sana Mhe. Zahra na namshukuru sana Dkt. Mwinyihaji wameanza kuchangia kidogo kutoa ufafanuzi katika sekta zao.

Mhe. Spika, hoja nyengine iliyoibuliwa na wengi sana ni ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, hata mimi bandari ninaitaka. Zanzibar tutapiga hatua kama tutakamata maeneo mawili bandari na maeneo huru. Lakini ninataka nikwambieni ndugu zangu hatuko mbali, juhudi zetu za kupata bandari zinaendelea vizuri na nataka nikutonyeni tu Waheshimiwa Wawakilishi mambo yakikaa vizuri Mhe. Mwanasheria Mkuu akishaipitia MoU vizuri tuta-sign MoU wiki ijayo. Tunataka tujenge bandari kwa sababu ile tuliyokuwa nayo hatuwezi tukaitumia abiria na mizigo, na sisi tuko katika *position* nzuri Zanzibar ya kuweza kuwa na bandari na kuinua uchumi, tatalifanya hilo na ninakuombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi tuwe pamoja katika suala hili la ujenzi wa bandari. Na wala msio gope, msio gope kwamba bandari ya bagamoyo inakuja, kuna bandari ya Mombasa, kuna Bandari ya Dar es Salaam, kuna bandari ya Mtwara, kuna bandari ya Tanga, kuna bandari ya Msumbiji na *still* Zanzibar iko *top*. Ukiangalia idadi ya mizigo inayokuja Zanzibar na uangalie na mizigo inayokwenda kule basi sisi tunakaa vizuri tusio gope kabisa.

Mhe. Spika, hoja nyengine iliyozungumziwa ni uimarisha wa uwanja wa ndege wa Pemba. Nataka niseme tu Mhe. Spika, uwanja wa ndege wa Pemba tuufunguwe, nasema lazima tuufunguwe na ndio mkakati wa Serikali lazima Pemba ifunguliwe, kuna watalii wengi wanatoka Mombasa wanataka kuja Pemba kuangalia shughuli za utalii Pemba, kwa uwanja ule hatutaweza kupata watalii wa kutosha, tayari tumeshazungumza na wenzetu na mazungumzo yanaendelea katika kuufungua uwanja wa ndege wa Pemba. Lakini kwa kipindi hichi kifupi tumetenga shilingi bilioni 2.7, kwanza kuitia taa uwanja wa ndege wa Pemba ili inapotokezea dharura angalau usiku tuweze kutua. Lakini la pili tunataka kukamilisha *feasibility study* katika kipindi hiki kabla hatujaingia mwaka 2015 tunataka tuanze kazi ya kuufungua uwanja wa ndege wa Pemba, na hili hatulizungumzi maana yake kuna Wajumbe wengine wanafikiria tukija hapa Mawaziri tunapiga mayowe tu, *we are serious* sio kila

kitu hata chakula hakijaiva unaanza kupiga kelele aah! Sio Mawaziri hawa ambao tuko hapa, Mawaziri hawa wanapika chakula kikiiva ndio kinakuja. Kuna wenzangu wengine hapa tunataka chakula hakijaiva tuanze kuja kupiga mayowe hapa, kikiungua wewe ukishakaa ukumbini unasubiri chakula kikiungua utasemaje. Nakuombeni sana mutuamini, mutuamini! Tumeingia miaka miwili na nusu sasa hivi lakini mambo ambayo tumeyafanya ndugu zanguni sio madogo.

Mhe. Spika, ajira kwa vijana nimeshazungumza.

Mhe. Spika, kuimarisha uvuvi wa Bahari Kuu. Katika sekta mpya ambayo sisi tunaitazama ni hii ya uvuvi wa bahari kuu, lakini Mhe. Spika, lazima tukubali kuwa na uvuvi wa bahari kuu sio kama mimi nitoke Chukwani nielekee Mji Mkongwe, tunahitaji matayarisho, tunahitaji kuwa-*train* vijana wetu, tunahitaji kuwapatia vyombo ambavyo vitakavyofika kule, ingelikuwa suala la kutoka Chukwani kwenda Mji Mkongwe tu mimi ningelikwenda tu Mji Mkongwe nikarudi jioni nyumbani basi. Tumeanza maandalizi mazuri na ile azma ya Rais ya kuunda Wizara ya Uvuvi ndio hii, kwamba hii sekta imejificha inatakiwa ifanye kazi sasa hivi ionekane na iweze kuchangia.

Mhe. Spika, tumetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa meli za kuweza kufika bahari kuu, imezungumzwa sana milioni mia moja iliyoko Wizara ya Uvuvi sijui iko wapi, hizi fedha zimetengwa kwa ajili ya mafunzo na kununulia vifaa vyengine vidogo vidogo, tume-*train* vijana 30 China tumewapeleka, lakini ndugu zanguni Waheshimiwa Wawakilishi sidhani kama mnatafuta wapi pa kujenga ma-*fish farm* kwa ajili ya kufugia samaki, lengo letu hii sekta tunataka tuikamate ili iweze kutuchangia, hii sekta hii inaweza kufanya vizuri zaidi kuliko sekta ya utalii. Hii sekta sio *fragile* lakini utalii ni *fragile* ukiuchezea kidogo tu hauji. Hii sekta tunaweza kwenda wenyewe kuvua, kwa hivyo tumejipanga vizuri na tutaendelea kumuwezesha Mhe. Haroun ili vijana watakaokwenda katika sekta hii waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mhe. Spika, tayari ndugu zetu wafadhili wameshaweka shilingi milioni 337 kama ni michango yao kutusaidia katika sekta hii. Na hivi karibuni tu Mhe. Rais wa Zanzibar alivyokuwa China kule kuna Kampuni za China zinataka kuja hapa na vyombo, tunawasubiri na wakichelewa tutakwenda tena mimi na Mhe. Jihad tukawafuate pamoja na mzee yule anayetaka kwenda China na yeye.

Mhe. Spika, eneo jengine lililozungumzwa ni mchango wa sekta ya kilimo na ukuaji wake. Nilisema katika bajeti ya mwaka jana Mhe. Spika, kwamba nchi yoyote inayotegemea kilimo ni masikini, tukiona mchango wa kilimo unapungua katika pato la taifa kuna sekta nyengine inakuwa haraka. Na hili

ndio lengo, mchango wa kilimo uendelee kupunguwa ili sekta nyengine ziweze kuimarika hasa sekta ya viwanda, sekta ya huduma, sekta ya fedha. Kwa hiyo Mhe. Spika, kuna mmoja aliuliza hapa akasema mbona hajaona hayo mazao yalivyokuwa yamepungua, kuna mazao leo yamepungua, mpunga umepungua kutoka tani 23000 mpaka tani 6000 mwaka 2011/12, hizo sio takwimu zangu takwimu za Wizara ya Kilimo. Muhogo umepungua kutoka tani 273000 mpaka 192000. Ndizi zimepungua kutoka tani 110000 hadi tani 97000. Mahindi yamepungua kutoka tani 3000 mpaka tani 857 na viazi vitamu vimepungua kutoka tani 92000 mpaka tani 31000.

Kwa hivyo Mhe. Spika, tunaweza tukaongeza juhudi lakini na sekta nyengine lazima zikuwe zaidi. Hatuna ardhi ya kusema kwamba kilimo kiwe tegemezi. Mimi naendelea kushauri naendelea kuwashawishi wenzangu mazao ya biashara yana tija zaidi ni vyema tukaangalia kama unapata eka tatu tu ukapanda hiliki basi kuna tija zaidi kuliko eka tatu ukapanda mahindi, Kwa hivyo ni vyema tukaangalia nalo hilo vile vile.

Mhe. Spika, suala jengine lililoibuliwa ni mchango wa viwanda kwenye pato la taifa. Hapa Mhe. Spika, nataka niseme tu kwamba Waheshimiwa walikuwa wakali kidogo, wengi walihoji viwanda vya kokoto, wengi walihoji viwanda vya mikate. Hizo sio *classification* zangu, hivi viwanda vimekuwa *classified* katika *International Standard of Industrial Classification*, kimataifa ndio wamevi-define hivi ni viwanda. Kimataifa *bakery* ni *industry* kama wewe unaona *bakery* yako inatumia kuni mwenzako anatumia gesi, *modernise your bakery*, lakini hebu nambie leo Wazanzibari wangapi mtengeneze ile mikate ya Bakhressa mtakula nyie, si wengi hamli mnataka boflo zenu. Si mnataka boflo zenu hebu nambieni. Kile ni kiwanda ukikikataa kiwanda cha mkate maana yake umekataa kiwanda cha biskuti, hivyo vyote ni viwanda vimekuwa *classified* kimataifa na wala sio mimi, na viwanda vya kokoto navyo ni viwanda, sema wewe una *crusher* yako ambayo ni *local* na mwenzako ana *modern*. Wapo hapa ma-*civil engineer* hapa Mhe. Hamad hebu nambie Kenya hawa-*export* kokoto, how many times tumenunua kokoto kutoka Kenya, Mhe. Hamad, waambie hawa, *how many times* Zanzibar tumenunua kokoto kutoka Kenya kwa ajili ya ujenzi, watu wana-*export* kokoto. Sasa mimi nashangaa Waheshimiwa tunapiga kelele kwamba kiwanda cha kokoto ndicho tulichonacho.

Mhe. Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wawakilishi kwamba juhudi tufanye za kutafuta viwanda zaidi na tayari tumeshaanzisha juhudi za kutafuta viwanda zaidi, pale Amani pale pana viwanda vya maji, kuna viwanda vya nguo, kuna viwanda vya kutengeneza vyombo vya plastiki, hebu katembeleeni jamani, na sasa hivi tunazungumzia kiwanda cha kutengenezea *fruit juice*. Lakini mimi nawasifu sana Waheshimiwa Wawakilishi Mhe.

Spika, baadhi yetu tunasafiri sana hapa na tukiwepo humu ndani tunasema sana kwamba nimeenda Marekani, nimeenda Barcelona nimeenda wapi lakini nakuombeni huko mnakokwenda waombeni wafanyabiashara waje waweze viwanda hapa. Tulikuwa na tatizo la umeme sasa hivi halipo, halipo tena tatizo la umeme sasa hivi. Kwa hivyo Mhe. Spika, *classification* ya sekta ya viwanda ina mchanganyiko wa *sub sectors* nne, moja ni hiyo ya uchimbaji mawe na madini, ya pili uzalishaji, ya tatu umeme, gesi na usambazaji maji, na nne ni ujenzi, hizo zote kwa pamoja ndio zina-*classify* sekta ya viwanda. Mhe. Spika, nimeagiza kitabu kimewekwa ofisini kule nilifikiria kwamba nitafanya *winding up* jioni lakini nitakuleteeni Waheshimiwa wanaotaka kukisoma hicho waangalie hizi *international classification*.

Mhe. Spika, *ZRB* haikufikia lengo la ukusanyaji wa mapato. Mhe. Spika, nimeeleza awali kuna mapato mengine jamani tukiyachezea kidogo yatatoka, yatatukimbia. Ukitizama *statistics* za watalii na makadirio na ukitizama *statistics* ukilinganisha na mwaka 2011 kuanzia mwezi wa Saba watalii wamepungua mpaka umemalizika mwaka, linganisheni hizo takwimu. Hii ni kwa sababu sisi wenyewe, mtalii haendi pahala penye fujo, tumefanya fujo mara ya kwanza, tukafanya fujo tena mara ya pili.

Mwaka jana mwezi Mei kulikuwa kuna mkutano wa *African Development Bank* kule Arusha na mwaka juzi nili-*lobby* mimi ule mkutano ufanyike Tanzania wakati tuko Lisbon, mimi ndiye niliyewasilisha maombi ya Tanzania, Lisbon tukakubaliwa mkutano ufanyike Tanzania, Arusha. Mawaziri wengi na watendaji wengi waliohudhuria pale walikuja wakapeana mikono na sisi wakasema tunataka ku-*visit* na Zanzibar. Vurugu zinatokea tuko Arusha, wengine walinjia wakanambia *We are no longer going to Zanzibar*, hakuna mtu anayetaka kwenda kuweka roho yake kwenye matatizo tumeanza kupoteza, nasema amani na utulivu Mhe. Spika, ni muhimu sana bila ya amani mapato haya yatakuwa ndoto.

Ujenzi wa nyumba na makaazi mimi nimelipokea sana wazo hili na ninadhani Mhe. Hamza Hassan Juma ni shahidi, tumeanza mazungumzo na *ZSSF* kwa nini *ZSSF*? *ZSSF* ana maeneo, *ZSSF* ana wanachama ambapo moja ya jukumu lake ni kuwapatia makaazi bora wanachama wake kwa njia ya mikopo, *ZSSF* atashirikiana na hawa wafanyabiashara ili waweze pamoja hizo nyumba na hatimaye wakopeshwe wafanyakazi wetu. Na sisi tunasema kwamba hiyo mialiko ya kwenda kuzungumza na wafanyabiashara basi Makamu wa Pili wa Rais anasubiri itakapofika wakati na sisi tutaangalia chungu kama kipo tutampeleka akashiriki akawasikilize wafanyabiashara hao. Lakini tuna hamu na sisi tushirikiane na wenzetu wafanyabiashara kwa lengo la kuwekeza katika Sekta ya Nyumba na Makaazi. Kwa hivyo, ndugu zangu wa *ZSSF* hili

tayari wanalo na wanasubiri, tumeambiwa wapo hawa wa Marekani, wako wengine kutoka Singapore wote tunawasubiri sisi.

Kuhusu malipo ya kodi kupitia benki. Nataka niseme tu Mhe. Spika, *TRA* na *ZRB* sasa hivi haziendi kwenye vikapu tena kodi zao, *ZRB* pale pale kuna benki ya *PBZ* mle mle ndani. *Airport* vile vile kuna kituo, sasa hivi *ZRB* hawaendi kwenye kikapu. Tatizo tulilionalo sasa ni mapato ya *visa*, nalo nataka niwahakikishieni dawa yake iko ukingoni, tumeshalifanyia kazi kwa kina, tumeshafanya *assessment* kwa kina, tumeshafanya *study* kwa kina, sasa hivi wataalamu wanaangalia jinsi ya kufunga vifaa ambavyo vitasaidia, hakuna mtu atakayechezea pesa ya *visa* pale, watu wataotumia *visa card* zao kulipia *visa*. Tunafunga vifaa sasa hivi kwa kushirikiana na Benki ya *CRDB*.

Vile vile tutajitahidi Mhe. Spika, mapato ya Halmashauri, Manispaa na Mabaraza nao vile vile walipie kupitia benki. Tukimaliza bajeti yetu hii nitamuomba Katibu Mkuu akutane na Maafisa Tawala pamoja na Wakurugenzi wa Manispaa ili alizungumzie hili suala na baadae tutatoa *circular* kuwataka wafanye hivyo. Hili linawezekana, Mhe. Waziri pale alikuwa anauza ving'amuzi akawaambia kila mtu akalipe deni aje na risiti tu hapa achukue king'amuzi na limewezekana. Kwa hivyo na hili vile vile Mhe. Spika, tutalitolea *circular* baada ya kukutana na wenzetu ili tuone kila mmoja sasa awe analipia benki.

Pia limezungumzwa suala la malipo yote *GBS* na *PAYE* kumejitokeza nini mpaka leo hatujazipata? Nataka niseme kwa kifupi tu wenzetu wale kwa upande wa *PAYE* tulikuwa tumeshamaliza na zimeanza kutoka vizuri tu mwezi wa Julai, Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba, Disemba, Januari, Februari zimetoka vizuri tu, 1.75 bilioni kwa mwezi. Kumbe ile *volt* ambayo wenzetu wameweka wanayopitishia hizo pesa kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais *volt* imekuwa ni ndogo. Kwa hivyo, wameshindwa sasa kupitisha pesa pale mpaka waanze kufanya uhaulisho na ndio maana ikawa pesa hizi hazikuweza kuja mpaka walipomaliza mwezi wa Mei wameanza tena. Bado tunazifuatilia miezi mitatu ile na mimi kwa uhusiano wetu wa karibu baina yangu na Dr. Mgimwa nina uhakika kwamba fedha hizo tutazipata wala sio jambo la kutushtua, kwa sababu ni haki yetu na tumeshakubaliana zitapatikana.

Bajeti ya Sekta ya Afya ni ndogo Mhe. Naibu Waziri wa Afya ameeleza wala sina haja ya kufafanua, ameeleza kwa kina. Malipo ya leseni za njia kupitia kwenye mafuta ni kumuua mwananchi. Hapa nataka niseme kidogo Mhe. Spika, ili kila mmoja aweze kunifahamu. Kwanza kodi yoyote ile tusijidanganye inalipwa na mwananchi, wala tusijidanganye kusema kodi hii, hii, kodi mlipaji ni mwananchi. Sasa hatua hii tuliyoiweka ina sababu zake; la

kwanza, tumegundua kuna risiti feki nyingi sana za *road license* na tunaozitengeneza ni sisi Wazanzibari, tukasema aa tukiendelea na utaratibu huu wa kutoa *road license* tutaumia.

Lakini la pili tukasema kwamba kwa nini anayetumia barabara sana asilipe sana, yule anayetumia barabara kidogo akalipa kidogo? Nilikuwa natoa mfano hapa Wawakilishi kutoka Pemba mnakuja hapa mna magari yenu mkishamaliza wiki mbili mnakwenda zenu kule majimboni Pemba gari mnazilaza na mimi niko hapa kila siku natembelea gari wewe ya kwako umeilaza kwa nini tulipe sawa *road license*, hakuna msingi wa kulipa sawa sawa. Tukasema mimi ninayetumia zaidi nitatia mafuta zaidi. Kwa hivyo, kila lita moja niweke shilingi 35 halafu kule *road license* naifuta, kule hakuna *road license* tena.

Sasa jana watu wamefanya mahesabu wakapiga kelele lita kumi, lita kumi, lita 10 shilingi 350 ndizo zilizowekwa na kwa wale wanaoendesha magari hapa lita 10 unakwenda Pwani Mchangani na kurudi kwa gari ambayo imepakia watu 20 kila mmoja shilingi mbili, maana yake wakati mwingine wazee tukikaa tukipiga kelele tufanyeni mahesabu, lakini yule ambaye ana abiria wengi kwenda na kurudi na yule ambaye mwenye shughuli nyingi za kwenda na kurudi ndiye anayetumia barabara sana. Kwa hivyo, mimi nikitumia lita 10 kwa siku moja nitaongeza shilingi 350, nikikuulizeni miaka mingapi hamjaiona shilingi hamsini nyinyi, mtasema hamjaiona na yule ambaye anataka kutumia gari kila siku zaidi ya lita 30 maana yake anakwenda mbali hiyo anatomia sana barabara kwa hivyo na huyu alipe sana.

Hoja yetu Mhe. Spika, ni kwamba hizi shilingi 35 kwanza tunafuta ile *road license* ya kwenda kule mkapewa *sticker* tunafuta. Lakini hizi zote mlizokuwa mkipiga kelele Waheshimiwa Wawakilishi zote zitachangia shilingi 124 milioni tu lakini tutakuwa tuna mapato ya uhakika hakuna atakayefoji *road license* ile *sticker* mapato ya uhakika sasa serikali itakuwa inapata na hakuna atakayekuwa analalamika gari yako ukisafiri unaiweka hutotumia barabara miezi miwili basi mchango wako kwenye *road license* utakuwa ni mdogo na ile ambayo kama mimi kila siku anakwenda anarudi mchango wake huyu wa *road license* utakuwa ni mkubwa. Kwa sababu hizi barabara lazima zijengwe na hatuwezi tukazijenga barabara hizi kwa wadanganyifu kutufanyia *road license fake*. Hoja yetu ndio hiyo Mhe. Spika.

Kwa hivyo, nina imani Waheshimiwa Wawakilishi kwamba sasa ndio tutapata mapato yetu na ile *value for money* itaondokana sasa, haiwezekani leo wewe ukapangiwa na mtoto mdogo ukaambiwa sahani hiyo kula na mtoto mdogo, wee utakula kingi kuliko yeye kwa nini ule kingi kuliko yeye, kwa

sababu wewe ndiye uliyekileta. Na kwa upande wa gari nayo hivi hivi yule anayetumia zaidi barabara ndiye alipe zaidi.

Suala jengine ambalo limeleta utata mkubwa sana Mhe. Spika, ni suala la kumruhusu mwekezaji mmoja aingize mafuta. Nimesikia wengine wananong'ona humu aa anataka kupewa fulani aingize mafuta peke yake, hapana Waheshimiwa Wawakilishi huu ndio mradi mkubwa tunataka tuufanye. Hivi sasa tuna makampuni nne, Kampuni za Kimataifa tatu na kampuni ya *local* moja wanataka kuweka matangi makubwa sana hapa Zanzibar ambao wataleta mafuta kwa meli kubwa sio hivi vidau, vimeli vidogo vidogo, wataleta mafuta kwa meli kubwa watamwaga kwenye matangi yale watauza ndani halafu watauza na nchi za karibu, wala msishangae mkasema haiwezekani.

Kenya hawazalishi mafuta hata lita moja lakini wanauza mafuta, Zanzibar *strategically* iko pahala pazuri, hizi nchi zote Burundi, Rwanda, zote tunaweza tukazisafirishia mafuta kutoka Zanzibar. Huyu atakua ni *only one importer*. Lakini Waheshimiwa Wawakilishi nataka nikudokoleeni tena jengine ile kunusanusa yetu kwamba Zanzibar kuna mafuta tukishachimba mafuta matangi yapo, matangi yatakuwa yameshawekwa hapo tayari. Kwa hivyo ni mpango wetu huo sasa hivi tutakuja tuyafungue zile kampuni nne tuzitizame nani mwenye uwezo halafu tumwambie fanya kazi maeneo tunayo ya kuweka matangi. Leo matangi haya tuliyonayo hapa mara ngapi jamani tunaambiwa mafuta hakuna nchini, tuna kampuni tatu zinazoleta mafuta inafika pahala tunaambiwa mafuta hakuna.

Nakumbuka siku moja sijui nilikuweco wapi nikapigiwa simu na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati akaniambia bwana mafuta hakuna nchini, nikamwambia sasa wee Mhe. Waziri mimi sizalishi mafuta, kampuni tatu hizo kwa sababu *storage capacity* haipo hapa. Kukitokea vurugu huko Mwenyezi Mungu apishie mbali miezi mitatu tu Zanzibar hamna mafuta kwa *storage* ile, huu ndio mpango wetu na wala hatuna nia ya kusema kwamba kuna mtu mmoja tunataka kumpa wala huyo hayumo kabisa ambaye anaomba, hayumo huyo mnayemfikiria nyinyi. Kwa hivyo, tupeni nafasi tufanye kazi, tunataka tufanye kazi na mambo tukifanikiwa mtaanza kuyaona haya matangi yanaanza kujengwa tuko *serious* katika hili. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk yupo?

Jengine lililozungumziwa Mhe. Spika, misamaha ya kodi kwa chakula hasa wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ikasemwa wengine wanapata taarifa mapema, sio hivyo. Mimi ndiye ninayehusika na misamaha ya kodi baada ya kupata barua kutoka kwa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na tukishapata barua kutoka kwa Mhe. Waziri wa Biashara huwa

tunazungumza na Mhe. Rais, sisi wengi ni Waislam Mwezi wa Ramadhan tunatoa unafuu kwa wananchi wetu; mchele, unga, tende, serikali nayo ina wajibu Mwezi wa Ramadhan angalau kutoa sadaka, sadaka yetu ni hiyo. Sasa mimi ninapotoa barua nampelekea Naibu Kamishna wa TRA kuanzia tarehe ya leo mpaka tarehe fulani, lakini tujue kwamba wafanyabiashara wengine inakuwa meli zao ziko njiani zinakuja, kwa hivyo yule anaweza akawahi kati kati ya barua yao haina maana kwamba amepata taarifa.

Lakini hebu tujiulizeni Mhe. Spika, hii Zanzibar kuna wafanyabiashara anaoleta mchele na unga wangapi? Wengine ni wachuuzi tu, ukimpa yeye taarifa kwa mfano Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi si mletaji mchele yeye ni mchuuzi tu, ukimpa taarifa yeye ataagiza mchele haraka haraka mchele alete na yeye wakati yeye si muagiziaji wa mchele ndio hao wanaolalamika. Lakini ukweli ni kwamba mimi siwezi nikamuarifu mfanyabiashara yoyote kwa sababu nikiwaarifu mchele utaingizwa mwingi hapa mtakula miaka miwili halafu nitakosa kodi, vyenginevyo tuteue wafanyabiashara wawili watatu halafu hao niwaarifu leteni basi iwe ndio wao. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hakuna hii.

Nikiendelea na umeme unaotokana na takataka. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alitaka nitoe taarifa ya umeme unaotokana na takataka. Huu umeme unaotokana na takataka sio wa serikali ni wa *private sector* na lengo letu ni kwamba watumie taka zetu za ndani ili kusafisha mji wetu kwa kuzalisha umeme. Taarifa tulizonazo ni kwamba wanakamilisha taratibu za kupata pesa wameshamaliza mazungumzo na *ZECO*, wameshamaliza mazungumzo na wizara, wanakamilisha taratibu za kupata pesa ili waweze kuja kuanza, tusubiri, tusubiri wala tusiwe na pupa kama kweli *they are serious* kama alivyo Mhe. Mshimba watakuja, kwa hivyo na mimi nawasubiri.

Mhe. Spika, suala jengine ni mapato yamezidi matumizi, tuangalie mimi nasema mahitaji yetu ni makubwa sana na wala sio serikalini tu, tusifike pahala Mhe. Spika, tukajidanganya mihimili yote mitatu hii. Mahitaji ya Baraza makubwa yamekua, mahitaji ya Mahkama yamekua na mahitaji ya Serikalini yamekuwa na wala tusijidanganye Mhe. Spika, tukasema kwamba tukipunguza Mawaziri ndio mahitaji yatapungua haya hayapungui, lakini nakubaliana na wale waliosema kwamba kubwa tuiangalie serikali yetu, watumishi 38000 mpaka 40000 kati ya *population* ya 1.3 milioni ni wengi lakini tutawapeleka wapi, ndio hii tunasema acha tutengeneze mazingira ya ajira ile aliyosema somo yangu ili wengine waondoke huku waende huku, lakini watu wanaona bora wakae ndani ya serikali kuna uhakika wa maisha yao kuliko kwenda kwenye sekta. Kuna *private sector* nyengine ikifika mwaka mmoja wanawatimua sasa hilo haliwezekani, serikali inatoa kima cha chini cha *private sector* analipa anavyotaka yeye hii haiwezekani. Nadhani

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika amenifahamu.

Kwa hivyo, matumizi sisi kwa upande wetu tayari tunalifanyia kazi hili suala kuangalia ni maeneo gani ndani ya serikali tunaweza tukakata matumizi yetu.

Sheria ya ZSSF irekebishwe ili wanachama waweze kuchukua fedha zao mapema wanapokuwa hawana ajira. Nasema zile fedha ni zako Mhe. Spika, mwanachama wa ZSSF anapokwenda kuweka pesa yake zile pesa ni za kwake, lakini unapokuwa una ajira ukasema sasa pesa zile unataka uzichukue dhumuni la mfuko limekuwa silo. Mfuko wa ZSSF maana yake nini? Maana yake unaweka pesa zako pale ili zije zikusaidie pale unapokuwa wewe hujiwezi tena hata kuajirika huajiriki, miaka 60, 65 Mhe. Haroun Ali Suleiman keshokutwa anakwenda kuchukua za kwake, miaka 60 tayari na mimi nikifika miaka 60 nitakwenda kuchukua za kwangu ili zije zitusaidie uzeeni ndio dhumuni lake. Lakini tunaliangalia hili katika marekebisho ya sheria ili Mfuko uweze kuwa endelevu lazima pesa zile zibakie pale vyenginevyo Mfuko mtauu na wewe utakufa.

Suala jengine Mhe. Spika, lilizungumziwa suala la kuwa tumejiandaaje, tumejipangaje na mabadiliko haya ya Katiba kama serikali. Nataka niseme kwamba ni mwezi uliopita ndio rasimu ya katiba imetoka. Kwa upande wetu nilimuona Makamu wa Kwanza wa Rais akipokea na sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu tumeshapewa nakala wengi wetu na ninaamini kwamba tumeanza kuipitia, Mawaziri wenzangu naamini wameanza kuipitia, bado kikao cha Baraza la Mapinduzi hakijakaa kuzungumza juu ya kujipanga kwa muelekeo wa Katiba mpya. Lakini ni imani yangu kwamba kila Waziri ameshaona maeneo ya kwake ambayo anahitaji kujipanga upya. Tunalifanya hilo kwa sababu kama mnavyojua katiba hii kama itakwenda kama ilivyopangwa tarehe 26 Aprili, 2014 itakuwa ndio inapitishwa. Kwa hivyo ni lazima tujipange na mimi nakubaliana na Wajumbe kwamba lazima tujipange ili hatimaye ikishapitishwa isiwe kama tumeshitukiziwa hivi. Kwa hivyo, hilo tumepokea ushauri na tutajipanga kwa udhati kabisa.

La mwisho Mhe. Spika, suala la miaka 50 ya Mapinduzi. Mhe. Spika, tunataka kuyaenzi Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Huwezi kuyaenzi Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 umetimiza miaka 50 unafanya shughuli zako kama vile umetimiza miaka miwili, mmoja, minne, kumi, hiyo 50 nusu karne. Kwenye sherehe zetu kama ilivyoelezwa na mimi nakubaliana na Wajumbe wote zive za Wazanzibari. Tushirikiane sote Wazanzibari katika kuzifanikisha sherehe zetu za miaka 50 na wengine wamekuwa na wasi wasi na matumizi ya fedha, msiwe na wasiwasi hakuna shughuli isiyokuwa haina gharama. Tufanye sherehe zetu za miaka 50 hapo ndio tutayaenzi Mapinduzi

ya mwaka 1964. Tuoneshe umoja wetu wakati wa sherehe zetu na wale wanaojilabu wana Mapinduzi basi wataonekana kama kweli ni wana Mapinduzi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa nimalizie kwa kutoa shukurani. Kwanza namshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuendelea kuniamini na kunivumilia katika nafasi hii na mimi namuahidi nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu kutekeleza majukumu yangu. Na pale ambapo nitakosea naomba wenzangu wanishitue.

Vile vile namshukuru sana Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais kwa busara zao wanazonipa kila wakati wanaponiita kunipa maelekezo na miongozo, nawaomba sana waendeleo kuniongoza.

Mhe. Spika, vile vile nakushukuru wewe kwa kuongoza vikao vyako vizuri na hatimaye kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho kwa ajili ya bajeti yetu hii. Lakini kikao chako hakitakuwa kizuri na hakitanoga kama Wajumbe hawa hawajaipitisha bajeti hii. Katika shukurani zangu natanguliza kwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba bajeti hii tuiptishe. Na mimi nakushukuruni sana, michango yenu ilikuwa zaidi inajenga haikuwa ya kejeli, mana kuna vyombo vyengine jana vimeripoti ovyo sana, wanasema ‘Wawakilishi waikandia bajeti’, mimi sijaona kama wameikandia hapa, mmeichangia vizuri, mmetuelekeza vizuri, Mawaziri na mimi nimepokea maelekezo yenu. Kwa hivyo, nakushukuruni sana.

Nawashukuru sana wananchi wa Zanzibar kwa uvumilivu na utulivu wao nawaomba waendeleo kudumisha amani ya nchi yetu na tija ya amani yetu itaonekana. Maendeleo yanapigwa kwanza kwa amani, nawashukuru sana watu wa Zanzibar.

Vile vile nataka nimshukuru sana mke wangu Bi Nariman Nassor Mohammed About kwa kunitunzia familia yangu. Nawashukuru na ninawapongeza sana na ninamwambia bado nampenda mke wangu, wale wanaolalamikia wake wanne basi mimi wangu mmoja lakini namshukuru sana. (*Kicheko*)

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo na shukurani hizo naomba sasa kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kutoa ufafanuzi. Imani yangu ni kwamba makofi mengi

hayakuwa ya kejeli, isipokuwa ni ya kuunga mkono. Baada ya hoja hiyo kutolewa na Mhe. Waziri basi nichukue nafasi hii sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KUAKHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Spika: Nichukue nafasi kuwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi zenu nzuri na ninayo taarifa kwamba Mswada unaofuata mara baada ya shughuli hii mpaka jana usiku mnamo saa tano Mhe. Waziri pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Wenyeviti wamekuwa wanashughulikia kiasi cha kwamba kuna baadhi ya mambo yanawekwa vizuri.

Hivyo, sitaki nimwambie Katibu kwamba tunaendelea na shughuli inayofuata ila nimuombe Mhe. Waziri mmoja wapo basi kwa mnasaba huo, na kwa kweli hii ratiba yetu ndivyo inavyoelekeza basi tuombe Wajumbe kama watakubali shughuli zetu tusitishwe hapa na tuje kesho. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa sababu shughuli zilizopo mbele yetu bado hazijakamilika, na kwa sababu Kamati inayohusika bado inaendelea kushughulikia mswada ambao ulikuwa uwasilishwe mara baada ya hoja ambayo imeshapitishwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Kwa hivyo, kwa sababu ya kuwapa nafasi Kamati inayohusika ya Baraza la Wawakilishi kumalizia kazi ambayo iko mbele yetu, naomba Baraza lako litengue Kanuni ya muda na tuweze kuakhirisha Baraza lako tukufu kabla ya wakati wake hadi kesho saa 3:00 asubuhi. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuakhirisha shughuli zetu kwa leo naomba nitoe tangazo moja. Kwa kweli kama tulivyoielezwa jana kwamba mwenzetu Mhe. Amina Iddi Mabrouk amefiliwa na mama yake mzazi na tunategemea maziko yatakuwa leo mnamo saa kumi za jioni, maiti itasaliwa Msikiti wa Masjid Noor Muhammad na hatimaye atakwenda kulazwa pale Mwanakwerekwe.

Kwa hivyo, tunaombwa Waheshimiwa Wajumbe tushiriki katika maziko ya mama yetu huyo na tumuombee Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi, amin.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe sasa niakhirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 20 Juni, 2013 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 6:05 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 20/06/2013 saa 3:00 za asubuhi)*

